



Tanzania Forest
Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi
Misitu ya Asili Tanzania



THE CENTER FOR
PEOPLE AND FORESTS

KIONGOZI CHA MAFUNZO

Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) na
Mpango wa Upunguzaji wa Hewa ya ukaa
inayotokana na ukataji wa miti hovyona
Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI):

Matukio ya Mafunzo katika ngazi
ya kijiji Tanzania

Toleo la kwanza, 2010



Mradi wa MKUHUMI kwa ajili ya Jamii na Uhifadhi wa Misitu Tanzania

Kiongozi hiki kimetayarishwa kupitia mradi wa “**Mradi wa MKUHUMI kwa ajili ya Jamii na Uhifadhi wa Misitu Tanzania**”. Mradi unalenga kupunguza uzalishaji wa gesi joto kutokana na ukataji wa miti hovyonyo na uharibifu wa misitu nchini Tanzania katika njia ambazo zinatoa motisha yenye usawa wa moja kwa moja kwa jamii zinazosimamia misitu kwa njia endelevu. Mradi unategemea kufanikisha hili kwa kusaidia uanzishaji wa Taasisi ya kijamii ya uuzaji wa Kaboni ambayo itakuwa chini ya Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu unaohusika na Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Taasisi hii itakusanya mauzo ya hiari ya upunguzaji wa gesi joto kutoka kwa wanachama wake na kuuza katika soko linalotambulika kwa viwango vya kimataifa. Kiasi cha fedha za mradi na mauzo ya kaboni sokoni yatapelekwa moja kwa moja kwa jamii kwa kuzingatia ubora wa matokeo hivyo kuongeza kiwango cha motisha wakati huohuo kuendeleza misitu na kupunguza ukataji wa misitu. Mradi unajumuisha sehemu ya tathmini na mawasiliano iliyoundwa kupata mafunzo yanayotokana na utekelezaji wa mradi na kutoa taarifa kwa jamii ya kitaifa na kimataifa. Mradi pia unalenga kujenga uwezo wa ndani kitaifa kuhusiana na MKUHUMI katika ngazi mbalimbali. Hii inahusishwa na mkakati wa Uraghibishi unaolenga kuunda njia nyepesi ya kutekeleza MKUHUMI nchini kwa kujihusisha katika uundaji wa miongozo na michakato ya MKUHUMI katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Mradi ni wa miaka 5 ambayo inaanza Septemba 2009 hadi Agosti 2014. Ni mradi wa ubia baina ya Shirika la kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA). Mradi huu umefadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya nchi ya Norway.

Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea:
<http://www.tfcg.org/makingReddWork.html>

© Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Kwa rejea:
TFCG 2011. Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) na Mpango wa Upunguzaji wa Hewa ya ukaa inayotokana na ukataji wa miti hovyonyo na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI): Matukio ya Mafunzo katika ngazi ya kijiji Tanzania, Taarifa ya kitaalamu TFCG 30. uk 1 – 64. Dar es Salaam.

YALIYOMO

YALIYOMO	III
VIFUPISHO	IV
SHUKURANI	V
SEHEMU YA 1: UTANGULIZI	1
SEHEMU YA 2: MODULI ZA MAFUNZO	5
MODULI YA 1: USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU (USM)	5
<i>Kipindi cha 1: Utangulizi na Mpangilio wa Mafunzo</i>	<i>5</i>
<i>Kipindi cha 2: Mahusiano yaliyopo kati ya misitu na watu</i>	<i>7</i>
<i>Kipindi cha 3: Majukumu ya jamii katika usimamizi endelevu wa misitu</i>	<i>10</i>
<i>Kipindi cha 4: Haki za Jamii katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM)</i>	<i>12</i>
<i>Kipindi cha 5: Kanuni Muhimu za Kufanikisha USM</i>	<i>14</i>
<i>Kipindi cha 6: Kuanzisha Usimamizi Shirikishi wa Misitu</i>	<i>17</i>
<i>Kipindi cha 7: Utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu</i>	<i>21</i>
MODULI YA 2: MPANGO WA KUPUNGUZA UZALISHAJI WA HEWA UKAA INAYOTOKANA NA UKATAJI WA MITI NA UHARIBIFU WA MISITU (MKUHUMI) NA MABADILIKO YA TABIA NCHI	26
<i>Kipindi 8: Ushahidi na chanzo cha mabadiliko ya Tabia Nchi</i>	<i>26</i>
<i>Kipindi 9: Vyanzo na namna ya kukabiliana na ukatiji wa miti</i> <i>na uharibifu wa misitu</i>	<i>30</i>
<i>Kipindi 10: MKUHUMI na hifadhi za kabon</i>	<i>36</i>
<i>Kipindi 11: Kuhitimisha na Tathmini</i>	<i>43</i>
SEHEMU YA 3: VIPINDI VYA NYONGEZA	44
<i>Uanzishaji wa vikundi</i>	<i>44</i>
<i>Vichangamsha mwili</i>	<i>44</i>
SEHEMU YA 4: VIAMBATISHO	46
<i>Kiambatisho cha 1. Maelezo</i>	<i>46</i>
<i>Rejea</i>	<i>48</i>
<i>Kiambatanisho cha 3. Mfano wa ratiba</i>	<i>49</i>

VIFUPISHO

CDM	Mfumo wa Maendeleo Salama
CFR	Hifadhi ya Misitu ya Jamii
COP	Mikutano ya Nchi Wanachama
DANIDA	Shirika la Maendeleo ya kimataifa ya Nchi ya Denmark
FAO	Shirika la Chakula na Kilimo
FBD	Idara ya Misitu na Nyuki
FTI	Chuo cha Mafunzo ya Misitu Olmotonyi
GHG	Gesi Joto
IPCC	Mkutano wa serikali za mataifa juu ya Mabadiliko ya Tabia nchi
MCDI	Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo
MJUMITA	Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Uismamiziwa Misitu Tanzania
MKUHUMI	Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Gesi Ukaa inayotokana na Ukataji wa miti na Uharibifu wa Misitu.
MRV	Ufuatiliaji, Taarifa na Uthibitishaji
PES	Ulipiaji wa Huduma za Mfumo Ekolojia
REAP	Mradi wa Kuhifadhi Mazingira Milima ya Rubeho
RECOFTC	KItuo cha Mafunzo ya Misitu kwa Jamii kwa Kanda ya Asia na Pasifiki
TFCG	Shirikala Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania
UMJ	Usimamizi wa Misitu ya Jamii
UNFCCC	Mpango wa Kimataifa wa Makubaliano wa Mabadiliko ya Tabia nchi
USM	Usimamizi Shirikishi wa Misitu

SHUKURANI

Kiongozi hiki cha mafunzo kimetayarishwa kupitia ushirikiano baina ya Shirika la kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na Kituo cha mafunzo ya misitu jamii katika nchi za Asia na Pasifiki (RECOFTC). Uundaji wa kiongozi hiki umefadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya nchi ya Norway kupitia mradi wa “MKUHUMI kwa ajili ya Jamii na Uhifadhi wa Misitu Tanzania”.

Tungependa kutoa shukurani za dhati kwa Ronnakorn Triraganon, Afisa Mkuu wa Programu, RECOFTC, juhudi na uvumilivu wake wakati wa utayarishaji wa kiongozi hiki unathaminiwa sana. Pia shukurani kwa Bettie Luwuge, Meneja wa Mradi wa MKUHUMI wa TFCG na MJUMITA, Someni Mteleka, Jofa Timanywa, Chikira Hassan, Nuru Nguya, Emmanuel Lyimo, Raymond Nlelwa, Wilfred Pima, Hamza O. Nkumulwa, Enos Kitumbika, Elisha Pallangyo na Charles Leonard wa TFCG na MJUMITA kwa michango yao muhimu wakati wa kutayarisha kiongozi hiki. Shukurani pia ziwaendee Othmar Haule, Charles Mwaipopo, Stanford Mahimbo and Sebastian Malisa kutoka Halmashauri za Wilaya za Kilosa na Lindi pamoja na Joseph Makero na Mhuji Kilonzo kutoka Chuo cha Misitu cha Olmotonyi na Gloria Massao kutoka MCDI. Shukurani pia zimwendee Nike Doggart, Mshauri Mkuu wa TFCG kwa kuhariri kiongozi hiki pamoja na Athuman Mgumia kwa kutengeneza michoro ya kurahisisha utumiaji.

Shukurani za dhati ziwaendee wanajamii wa vijiji vya Dodoma Isanga, Chabima na Illonga kutoka Wilaya ya Kilosa kwa michango yao wakati wa kuboresha na kufanyia majaribio kiongozi hiki. Haitowezezana kutaja kila mmoja alieshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha utayarishaji wa kiongozi hiki lakini juhudi mbalimbali zilizotumika kufanikisha kazi hii zinathaminiwa sana.

DIBAJI

KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI WA SHIRIKA LA KUHIFADHI MISITU YA ASILI TANZANIA

Ukataji wa misitu uliokithiri katika maeneo mengi hapa nchini Tanzania unapelekea upotevu wa rasilimali muhimu kwa mamilioni ya watu pamoja na kusababisha upotevu wa bioanuwai ya thamani sana ambayo hairudishiki; uharibifu wa huduma ya mifumo ikolojia mingine, na kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi joto katika anga. Upunguzaji wa gesi joto inayotokana na ukataji wa miti hovyo na uharibifu wa misitu (MKUHUMI) katika nchi zinazoendelea ni njia moja wapo inayowezekana kukabiliana na upotevu wa misitu nchini Tanzania. MKUHUMI unaweza kutoa njia kwa jamii za vijijini kuachana na shughuli ambazo zinasababisha ukataji wa misitu na uharibifu wa misitu kama inaweza kufanyika katika njia ambayo ni madhubuti na thabiti.

Ili MKUHUMI uweze kufanikiwa, hasa katika nchi kama Tanzania ambayo asilimia 70 ya ardhi inachukuliwa kama Ardhi ya kijiji, ushirikishwaji wa wanajamii ni muhimu sana. Tanzania imekuwa mstari wa mbele kwenye usimamizi shirikishi wa misitu barani Afrika. Sera ya Taifa ya misitu inawapa fursa jamii kusimamia misitu yao wenyewe pamoja na kuhamasisha ushirikishwaji katika usimamizi wa misitu ya hifadhi ya serikali za mitaa na serikali kuu.

Kiongozi hiki kinatazamia kuongoza wakufunzi namna dhana, kanuni na utendaji wa MKUHUMI unavyoweza kutambulishwa kwa wanakijiji kwa mtazamo wa sera ya taifa ya misitu katika mlengo wa usimamizi shirikishi wa misitu. Kiongozi hiki kinatambulisha usimamizi shirikishi wa misitu na MKUHUMI na kutoa mwongozo kwa wawezeshaji namna ya kujumuisha katika programu za ufundishaji ambazo ni shirikishi na za kiutendaji. Kiongozi kinazingatia mbinu za elimu ya watu wazima na mbinu za kujengea uzoefu. Kiongozi kimefanyiwa majaribio na kujengea kwenye uzoefu mpana ambao RECOFTC imepata kwa miongo ya kufanya kazi katika nyanja za kujenga uwezo katika masuala ya misitu barani Asia na Pasifiki

Kiongozi hiki pia kinapatikana katika lugha ya kiingereza kwenye <http://www.tfcg.org/publications>. Kiongozi kwa ajili ya mafunzo ngazi ya Wilaya pia kinapatikana katika lugha ya kiingereza na Kiswahili. Toleo la kiingereza limetayarishwa kwa ajili ya watumiaji wengine wasiotumia Kiswahili na wangependa kujifunza uzoefu wa Tanzania. Kwa kuwa MKUHUMI ni dhana ambayo inaendelea kubadilika siku hadi siku tutakuwa tunaboresha kiongozi hiki mara kwa mara ili kujumuisha mabadiliko muhimu kwa hiyo tafadhali tembelea tovuti yetu kwa ajili ya toleo lenye maboresho. Tafadhali pia tungependa kupata mrejesho kutoka kwako kuhusu kiongozi hiki na maoni pamoja na mapendekezo yako.



Charles Meshack

Mkurugenzi Mtendaji,

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG)

tfcg@tfcg.or.tz

Utangulizi wa Kiongozi

Jinsi ya Kutumia Kiongozi hiki

Kiongozi hiki kinatumia mbinu shirikishi za ufundishaji kwa kuzingatia kanuni za kujifunza kwa kutumia uzoefu kwa watu wazima. Vipindi vimelenga kuwa shirikishi ili kuwezesha washiriki kujifunza zaidi. Kwa namna hii uzoefu wa washiriki unakusanywa ili kupata mambo mapya ya kujifunza. Toleo la Kiongozi hiki kimsingi limewalenga wanakijiji, toleo lingine limewalenga watendaji wa Wilayani ambalo pia linaweza kutumika kuwajengea uwezo wasimamizi wa miradi, watunga sera, wasomi na wenye taaluma nyingine wenye nia ya kujifunza USM na MKUHUMI.

Maandalio ya vipindi ndani ya Kiongozi hiki yameundwa kwa utumiaji wa siku nne za mafunzo kwa kuongelea mambo ya msingi ya USM na MKUHUMI. Maandalio yamepangwa katika mtiririko maalumu. Hata hivyo unaweza kutumia kama ilivyo au kurekebisha kutegemea na mahitaji yako. Unaweza pia ukahitaji kuendelea kwa undani zaidi wa Kiongozi hiki ili upate mawazo zaidi na vitini. Vipindi vilivyowasilishwa katika Kiongozi hiki vinatoa mfano; kwa kufanya rahisi zaidi na kwa ubunifu wako mwenyewe kinaweza kukusaidia kuunda programu yako ya mafunzo.

Katika kutumia Kiongozi hiki kwa ajili ya mafunzo katika nchi nyingine au kwa lugha nyingine, ni vizuri ukaangalia kwa umakini tafasiri ya baadhi ya misamiati ya kitaalamu inayoendana na MKUHUMI na USM. Pia kuna mambo mengine yanaweza kutumika au kurekebisha kuendana na hali halisi ya maeneo husika kama vile viburudisho vya mwili na desturi.

Namna Kiongozi kilivyo pangwa

Kiongozi kimepangwa katika sehemu kuu nne.

Sehemu ya Kwanza inatoa taarifa za utangulizi kwa watumiaji kuhusu namna wanavyoweza kutumia Kiongozi hiki.

Sehemu ya pili inaelezea maandalio 12 ya vipindi vilivyo pangiliwa katika moduli tatu, moja ni kuhusu USM, moja juu ya MKUHUMI na moja juu ya mbinu za uwezesaji

Kila andalio la kipindi linajumuisha taarifa kuhusu:

- Malengo ya kipindi;
- Vifaa vinavyohitajika kuendesha na kukamilisha kipindi;
- Muda unaotakiwa kutengwa ;
- Hatua za kufundishia;
- Na baadhi ya maoni kuhusu kipindi cha mafunzo.

Moduli ya 1 inahusu Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM); moduli hii inaeleza hatua zinazohitajika wakati wa kuanzisha usimamizi shirikishi wa misitu kwa madhumuni ya usimamizi wa misitu ya jamii. Sehemu hii inatoa msingi wa sehemu nyingine katika Kiongozi hiki.

Moduli ya 2 inahusu Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji wa misitu na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) na mabadiliko ya tabianchi. Inatoa mlolongo wa vipindi vinavyotambulisha dhana ya MKUHUMI. Katika moduli hii, vipindi

pia vinaeleza mahusiano kati ya, MKUHUMI na USM. Inatoa fursa za kuchambua dhana za MKUHUMI, namna ya kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Moduli ya 3 inahusu mbinu za uwezeshwaji. Sehemu hii ina vipindi viwili vinavyohusu mbinu za uwezeshaji. Sehemu ya kwanza inaainisha mbinu za msingi za uwezeshaji na sehemu nyingine ya kipindi inaangalia namna mbinu hizi zinavyoweza kutumika katika hali halisi ya uwezeshwaji wa Usimamizi Shiriki wa Misitu (USM).

Sehemu ya tatu inatoa kipindi cha nyongeza kuhusu mrejesho wa mafunzo. Pia inajumuisha baadhi ya viburudisho na vichangamsho vya ziada.

Sehemu ya nne inajumuisha tafasiri ya maneno na orodha ya rejea.

Namna Kiongozi hiki kilivyotayarishwa

Kiongozi hiki kwa ajili ya mafunzo katika ngazi ya kijiji kuhusu Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na Ukataji wa miti na Uharibifu wa misitu (MKUHUMI) na usimamizi shirikishi wa misitu (USM) kilitayarishwa kutokana na ushirikiano wa pamoja kati ya watekelezaji kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali, watumishi wa serikali za mitaa na Chuo cha Misitu cha Olmotonyi kilichoko chini ya Idara ya Misitu na Nyuki. Kilianzishwa wakati wa warsha iliyoandaliwa na TFCG na MJUMITA mwezi Mei 2010. Kiongozi kwa ajili ya mafunzo kwa Ngazi ya Wilaya kiliandaliwa. Kwa jumla, warsha nne zilifanyika na kuwashirikisha washiriki walewale ili kuweza kutayarisha Kiongozi hiki. Kiongozi kilifanyiwa majaribio kwa kuendesha programu ya mafunzo kwa vijiji vitatu katika Wilaya ya Kilosa. Vijiji hivyo ni Dodoma Isanga, Ilonga na Chabima. Maoni na mrejesho chanya kutoka kwa wadau wa vijiji hivyo yalivyotokana na mafunzo ya majaribio yalijumuishwa. Pia michoro iliongezwa



Kujitayarisha kwa ajili ya mafunzo

Kutumia mafunzo kwa washiriki wenye historia tofauti

Katika sehemu hii, tumeweka pamoja baadhi ya mambo muhimu tuliyojifunza na mapendekezo yaliyojitokeza wakati wa majiribio ya Kiongozi hiki na kutokana na uendeshaji wa zoezi kama hili nchi nyingine.

Uwe wazi kuhusu malengo yako ya mafunzo: kama utatumia Kiongozi hiki, uwe na uhakika wa kuwa na malengo yaliyo wazi na ya kueleweka na kuweka malengo yenye uhalisia. Uwazi wa malengo ya mafunzo unasaidia washiriki kuelewa nini kinachotarajiwa kutoka kwao.

Chagiza mawazo ya kisasa kuhusu mafunzo bila kuanzisha upinzani: ili kuhamasisha washiriki kutumia mbinu za mafunzo zilizoainishwa katika Kiongozi hiki, unaweza kuhitaji kuwauliza mawazo yao kuhusu ufundishaji. Hii ni muhimu ikafanyika kwa uangalifu ili watu wote wawe pamoja. Kwa mfano, dhana zinazohusu kanuni za elimu ya watu wazima, jukumu la mwezeshaji ni kutoa changamoto kwao, kujifunza kwa uwazi zaidi, mrejesho chanya, viburudisho na michezo inaweza kuwa mipya wa washiriki wako. Hata hivyo, unaweza kuhitaji kurekebisha baadhi ya vipengele ili washiriki wako waweze kuzihusisha.

Tumia misamiati ya mafunzo kama ilivyotumika katika Kiongozi hiki: Misamiati ya mafunzo katika Kiongozi hiki imechaguliwa kwa umakini. Inaendana na filofia ya mafunzo shirikishi na kujifunza kwa uzoefu kuelewa baadhi ya mitazamo iliyopo katika utoaji wa mafunzo ya kawaida. Hivyo basi, usitumie misamiati iliyozoeleka katika mafunzo ya kawaida hata kama inajulikana zaidi, kwa sababu inaweza kueleweka tofauti. Badala yake tumia misamiati mipya na ueleeze maana yake. Kuna njia nyingi za utumiaji wa hii misamiati ya kigeni.

- Tafuta neno katika lugha yako au ya kienyeji inayokaribiana na maana halisi
- Kutunga neno jipya katika lugha yako na kuelezea maana yake.
- Kutumia neno la mwanzo la lugha hiyo na kufafanua maana kwa lugha inayoeleweka.

Maamuzi yatatofautiana kutoka eneo na eneo kulingana na uamuzi gani ni bora zaidi. Mfano: viburudisho, vichangamsha mwili, marudio ya sentensi.

Maandalizi mengine kwa ajili ya mafunzo shirikishi

Baadhi ya mipangilio ambayo inahitaji maandalizi maalumu wakati wa kuendesha mafunzo shirikishi.

- **Uchanguzi wa sehemu ya mafunzo**

Ingawa mafunzo haya shirikishi yanaweza kufanyika mahali popote, ni vizuri kuelewa baadhi ya mahitaji ya msingi ambayo yatasaidia kuendesha mafunzo haya kwa wepesi na kwa utulivu kwako na washiriki. Jambo la muhimu zaidi ni kuwa na eneo linaloweza kubadilika na lenye ubora. Kwa sababu washiriki watakuwa wana mizunguko, mwezeshaji atahitaji eneo la kutosha au chumba chenye ukubwa wa kutosha na samani zinazohamishika, kama vile meza na viti. Vipindi vingi katika Kiongozi hiki vinahamasisha washiriki kubadilishana uzoefu wao na maoni kuhusu USM na MKUHUMI, wakiwa wameketi mfano wa "U" au duara watakuwa na ushiriki kamilifu kuliko m.f watakapokaa mithili ya "kanisa"

- **Ununuzi la vifaa vya mafunzo na shajala**

Kwa vipindi vilivyoelezewa ndani ya Kiongozi hiki, utahitaji vifaa mbalimbali kama vile chati pindu, kalamu kubwa kwa ajili ya vikundi. Vifaa vinavyoweza kupatikana maeneo hayo vinaweza kutumika pia.

- **Kuweka kumbukumbu na taarifa za mafunzo**

- Uwekaji wa kumbukumbu za mchakato

Mara nyingi masuala ya mafunzo hayawi sahihi kwa mara ya kwanza unapoyaendesha, ungehitaji kuboresha kadri unavyoendelea. Njia nzuri zaidi ya kuyaendesha ni kwa kuandika kumbukumbu ya mafunzo husika mara kwa mara kuhusu kinachoendelea na kutafakari kilichofanyika. Unaweza kufanya hivyo wakati wa mapumziko, wakati wa jioni au kumuomba mtu (hususan msaidizi wa mafunzo) akusaidie. Ni muhimu kumbukumbu za mafunzo zifanyike haraka iwezekanavyo; mawazo bora ni yale yanayofanyika papo kwa papo.

- Uwekaji wa kumbukumbu za matokeo

Mijadala yote, ubadilishanaji wa uzoefu, mrejesho wa kila siku na mazoezi mengine katika vikundi vidogo vya kazi vitazalisha taarifa nyingi zenye thamani ya matokeo ambazo washiriki wangependelea kwenda nazo nyumbani. Kuandika taarifa za chati pindu ni kazi kubwa lakini ni jambo la umuhimu sana katika mafunzo shirikishi.

Njia zote za kumbukumbu zinaweza kufanyika katika njia mbalimbali na watu tofauti. Hata hivyo ni muhimu kufikiri kuhusu nini cha kuandika, kwa namna gani, nani anaweza kufanya na kiandae ipasavyo.

- **Muda**

Mtumiaji wa Kiongozi hiki cha mafunzo anashauriwa kuzingatia muda wakati wa mafunzo jambo ambalo litakuwa vyema kwa mshiriki pamoja na mwezesaji wakati wa mafunzo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba washiriki wanaweza kuwa wanahitajika katika shughuli nyingine kwa wakati huo.

Sehemu hii inaelezea vipindi 12 vya mafunzo vilivyo andaliwa katika moduli mbili:

- Moduli ya 1-inaongelea Usimamizi Shirikishi wa Misitū.
- Moduli ya 2- inaelezea MKUHUMI.

Moduli ya 1: Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM)

Kipindi cha 1: Utangulizi na Mpangilio wa Mafunzo	
MALENGO	Mwisho wa kipindi, washiriki... <ol style="list-style-type: none"> 1. Watakuwa wamefahamiana 2. Wataelewa malengo ya mafunzo na mada zitakazojadiliwa wakati wa mafunzo 3. Wataweka na kukubaliana taratibu za kufuatwa wakati wa mafunzo
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Chati pindu • Kalamu kubwa • Kadi za manila • Gundi • Kitini cha malengo ya mafunzo, • Kitini cha agenda za mafunzo • Malengo na agenda za mafunzo zilizoandaliwa kwenye chati pindu <p>Kalamu na daftari za kuandikia</p>
MUDA	Saa 1 na dakika 30
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi amkaribishe mwenyekiti wa kijiji kufungua rasmi matukio ya mafunzo. 2. Mwenyekiti wa kijiji awakaribishe wakufunzi kujitambulisha. 3. Mkufunzi anawambia washiriki kujitambulisha kwa kutaja majina yao, wadhifa wao katika kijiji (hususan katika kusimamia misitu) na kwa kutaja aina ya “udau wao” katika msitu m.f mganga wa jadi, mtengeneza mkaa, mvunambao, mkusanya kuni au mfugaji. 4. Mkufunzi agawe vipande vya karatasi na kuwambia washiriki kuandika majina yao kwenye vipande hivyo. 5. Mkufunzi atawaongoza washiriki kwa dakika 10 kupitia malengo ya mafunzo na mada zitakazofundishwa kwa siku nne kwa kutumia chati pindu zilizoandaliwa na mkufunzi. Ruhusu dakika 5 kwa ajili ya maswali na ufafanuzi. 6. Mkufunzi agawe shajala (vitabu vya kuandikia, kalamu na ratiba ya mafunzo) kwa washiriki. 7. Mkufunzi awezeshae uanzishwaji wa kanuni ndogo za kufuatwa wakati wa muda wa mafunzo. 8. Mkufunzi aandike kanuni kwenye chati pindu na kuwauliza washiriki kama wanakubaliana. 9. Mkufunzi awambie washiriki kujitolea kuunda timu ya mrejesho, timu ya huduma au timu ya burudani kwa kuwaeleza kuwa hizi zitabadilishwa kwa kila siku. Mkufunzi aelezee majukumu ya kila timu.

	<p>Timu ya mrejesho – kukusanya taarifa kwa kila mwisho wa siku na kuzichambua ili kuziwasilisha siku inayofuata.</p> <p>Timu ya huduma – itakuwa na jukumu la kuweka chati pindu kwenye ukuta, kugawa kadi na kalamu kubwa na kuainisha mtunza muda.</p> <p>Timu ya burudani - wanajukumu la kuburudisha na kuchangamsha pale inapohitajika.</p> <p>10. Mkufunzi aelezee kwa kifupi mbinu zitakazotumika kufundishia. Mkufunzi ataje kuwa mafunzo haya yanaweza kuwa tofauti na mafunzo mengine ambayo walishawahi kuhudhuria siku za nyuma. Katika mafunzo haya wanakijiji wanakuwa na fursa zaidi kubadilishana uzoefu, mawazo, maoni na mapendekezo ili mambo muhimu yanayotokana na mafunzo haya yaweze kwenda na hali halisi iliyoko kijijini.</p> <p>11. Mkufunzi aeleze kuwa kila kipindi kitakuwa kinajengea na kina mwendelezo kutoka vipindi vilivyopita. Kwa maana hiyo ni muhimu kuhudhuria vipindi vyote.</p> <p>12. Mkufunzi anajumuisha kipindi kwa kuwahamasisha washiriki kuongea na kutoa mawazo yao kadri wanavyoweza.</p>
<p>MAONI</p>	<p>Zoezi la kujitambulisha linaweza kuwasababishia baadhi ya washiriki kutojisikia vizuri hivyo uangalifu wakati wa kujitambulisha ni muhimu kuzingatiwa katika zoezi hili.</p> <p>Pia ni muhimu kuwakumbusha washiriki kuwa timu ya mrejesho itakusanya mrejesho na kwamba wajumbe wa timu hiyo watakuwa wanabadilika.</p> <p>Baadhi ya kanuni zinazopendekezwa;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Muda wa kuanza... muda wa mapumziko ya chai na chakula muda wa kumaliza... • Kila wazo liheshimiwe • Kutunza mazingira ya eneo la mafunzo • Kuzima simu au kuziweka katika hali ya mtetemo • Washiriki kuwa wachangamfu na kuchangia na wazingatie muda

Mafunzo kwa ngazi ya Kijiji kuhusu
 “Usimamizi Shiriki wa Misitu (USM) na
 Mpango wa Kupunguza Ukataji wa miti ovyo na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI)”

MALENGO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa mafunzo:

1. Washiriki watakuwa wanaweza kuelezea dhana za Usimamizi Shirikishi wa Misitu na Mpango wa Kupunguza Ukataji wa miti ovyo na Uharibifu wa Misitu na mahusiano yaliyopo kati yao.
2. Washiriki watakuwa wanaweza kufafanua hatua za kuanzisha Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM).

Siku ya 1	Siku ya 2	Siku ya 3
<ul style="list-style-type: none"> ○ Utangulizi wa Mafunzo yote ○ Mahusiano kati ya misitu na watu ○ Majukumu ya jamii katika usimamizi endelevu wa misitu ○ Haki za jamii katika usimamizi shirikishi wa misitu ○ Kanuni muhimu za kuwezesha mafanikio katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu 	<ul style="list-style-type: none"> ○ Hatua za uanzishaji wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu . ○ Utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ○ Ushahidi na vyanzo vya mabadiliko ya tabianchi. 	<ul style="list-style-type: none"> ○ Vyanzo na njia za kukabiliana na ukataji wa miti hovyoyo na uharibifu wa misitu. ○ MKUHUMI na hifadhi za kaboni. ○ Kuhitimisha na tathmini. ○ Kufunga.

Kipindi cha 2: Mahusiano yaliyopo kati ya misitu na watu


MALENGO	<p>Kufikia mwisho wa kipindi washiriki wataweza :</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuorodhesha na kuelezea namna watu wanavyofaidika kutokana na misitu na namna misitu inavyofaidika kutokana na watu.
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Chati pindu • Kalamu kubwa • Gundi • Kadi • Kitini: Mahusiano kati ya watu na misitu .
MUDA	Dakika 45
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi awaelezee washiriki kwamba kabla hawajajifunza kuhusu USM, watachambua kwanza namna ambazo watu wanafaidika na misitu na misitu inavyofaidika na watu. 2. Mkufunzi aeleeze kwamba watu na misitu wanategemeana sana. 3. Mkufunzi awagawe washiriki katika makundi 4 kwa kuhesabu 1 hadi 4, kila mshiriki mwenye nambari 1 ataunda kundi 1 na vivyo hivyo kwa 2, 3 na 4. 4. Elezea zoezi kwa kila kikundi ambapo kundi la 1 na 3 watajadili na kuchambua faida ambazo watu wanapata kutoka kwenye misitu wakati kundi la 2 na 4 watajadili na kuchambua ni kwa namna gani misitu inafaidika na watu. 5. Ruhusu kila kundi kuandika kila wazo kwenye kadi moja 6. Baada ya dakika 15, waambie kila kundi kuambiza walichojadili katika mawasilisho. Mawasilisho yaanza na makundi ya 1 na 3. Mawasilisho yafuatiwe na muda wa majadiliano na maoni kutoka kwa watu wengine. Washiriki wanapaswa kukubaliana kuhusu orodha ya faida zinazotokana na misitu. Hatua hiyohiyo kwa makundi yaliyobaki. Mkufunzi anaweza kuongeza mawazo mengine kama kuna mambo muhimu yanayopungua. Weka kadi zote kwenye chati pindu. 7. Toa muhtasari wa matokeo ya mawasilisho ya makundi. 8. Mkufunzi agawe kitini na kuorodhesha faida watu wanazopata kutoka kwenye misitu na misitu kutoka kwa watu . 9. Mkufunzi ahitimishe kipindi kwa kuwaambia kuwa watu mbalimbali wanaweza kuwa na thamani na faida tofauti kwenye misitu na misitu kutoka kwa watu na kwamba watu wanaweza kuiathiri misitu kwa njia mbalimbali. Baadhi ya hizi athari ni matishio kwa misitu. Kama tunataka kuendelea kupata faida hizi tunapaswa kupunguza matishio haya kama tutakavyojadili kwenye kipindi kinachofuata.
MAONI	

Misitu ni muhimu sana kwa watu na wanyama wengine. Kuna njia nyingi ambazo misitu inawapa faida watu pamoja na kuwezesha utoaji wa mbao, mijengo, kuni, mkaa, asali, hewa nzuri, maeneo ya kuabudia, miti shamba, chakula na makazi. Misitu pia inaweza kusababisha matatizo kwa watu kwa mfano kuhifadhi wanyama wanaovamia mashamba ya mazao ya kilimo.

Katika miaka ya hivi karibuni, maeneo makubwa ya misitu yamefyekwa na watu. Shughuli zinazosababisha misitu kufyekwa ni tishio kwa misitu. Shughuli hizi ni pamoja na moto, kilimo cha kuhamahama, ukataji wa miti bila kufuata njia endelevu, uchimbaji wa madini msituni, uwindaji haramu, uchomaji wa mkaa usiofuata utaratibu maalumu, na urinaji wa asali kwa kutumia moto. Watu pia wanaweza kuwa na jukumu kubwa sana la kuhifadhi misitu, kupitia upandaji wa miti, kuzuia moto, uhifadhi wa bioanuwai, kufanya doria, utekelezaji wa sheria na sera na elimu ya mazingira.

Mifano ya mambo watu wanayopata kutoka msituni

- Mbao
- Mijengo
- kuni
- madawa ya miti shamba
- chakula
- Shelter
- Destructive animals(wildlife)



Mifaano ya mambo ambayo misitu inapata kutoka kwa watu

- Moto
- Uharibifu wa misitu
- Upandaji wa miti
- Utengenezaji wa sheria na sera
- Uvamizi wa maeneo ya misitu
- Uchimbaji wa madini

Kipindi cha 3: Majukumu ya jamii katika usimamizi endelevu wa misitu

MALENGO	<p>Kufikia mwisho wa kipindi washiriki wataweza :</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kutambua nini wanakijiji wanaweza kufanya ili kusimamia msitu ili kuendelea kupata faida wanazozipata.
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Chati pindu • Kalamu kubwa • Gundi • Kitini: Majukumu ya jamii katika usimamizi endelevu wa misitu
MUDA	Saa 1
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi awambie washiriki kupitia faida za watu kutoka kwenye misitu na madhara watu wanayoweza kuwa nayo kwenye misitu kama ilivyoainishwa katika kipindi kilichopita kwa kuwauliza mtu mmoja mmoja kuzitaja. 2. Mkufunzi awashauri kwamba ili kuendelea kuwa na kufaidika na faida za misitu hatuna budi kuweka misitu katika hali nzuri na kupunga shughuli zinazotishia uwepo wa misitu. 3. Mkufunzi awambie washiriki waainishe shughuli ambazo zinaweza kulinda misitu. Washiriki wajigawe katika vikundi vidogo kulingana na idadi ya matishio yalioanishwa katika kipindi kilichopita. 4. Kwa dakika 20, vikundi vijadili namna ya kukabiliana na tishio moja. 5. Makundi yapeane matokeo majibu wakati wa mawasilisho. 6. Mkufunzi aandike majibu ya kila kundi kwenye chati pindu. Uliza maswali kwa ajili ya ufafanuzi inapobidi. 7. Baada ya kila kundi kuwasilisha matokeo yao, mkufunzi atoe muhtasari wa matokeo na kuwauliza kama wanakubaliana na mambo ambayo yametajwa kuwa njia zinazosaidia kuendeleza misitu yetu. 8. Mkufunzi ahitimishe kipindi kwa kuwahimiza washiriki kufanya kazi kwa bidii kupungunza matishio yaliyoanishwa na kutekeleza njia za kuyapunguza. Taja kuwa katika kipindi kijacho vikundi vitajadili zaidi kuhusu majukumu na haki za jamii juu ya rasilimali za misitu.
MAONI	<ul style="list-style-type: none"> • Kama kuna matishio mengi, mkufunzi anaweza kujadiliana na washiriki na kufanyia kazi matishio matano yatakayopewa kipaumbele. • Mkufunzi anaweza kutumia matokeo kwenye kipindi hiki kwenye kipindi cha 9 kuhusu “Vyanzo na njia za kukabiliana na ukataji wa miti hovyoo na uharibifu wa misitu” tena. • Matishio ya misitu ni pamoja na: Kilimo cha kuhamahama, moto, uchomaji wa mkaa, uvunaji wa mbao, uvamizi wa misitu, uchimbaji wa madini ndani ya msitu, ufugaji holela.

Jamii ina jukumu kubwa sana katika usimamizi wa misitu ili kuongeza faida zinazotokana na misitu na kupunguza matishio katika misitu. Baadhi ya njia ambazo zinatumiwa na jamii kupunguza au kuondoa matishio katika misitu ni pamoja na:

- Kufanya kilimo endelevu ikiwa ni pamoja na kilimo msitu na kilimo mseto.
- Kupunguza matumizi ya moto wakati wa kuandaa mashamba, kurina asali na kuwinda.
- Kufuata taratibu za kisheria na sheria ndogo za usimamizi wa misitu
- Kulinda rutuba kwenye ardhi katika mashamba yao hivyo kupunguza hitaji la kufungua mashamba mapya msituni.
- Kupanda na kulinda miti iliyopandwa katika maeneo yao ndani ya kijiji.
- Kuhakikisha kwamba mazao yanayotokana na misitu yanatumika kwa njia endelevu
- Kusaidiana katika kupunguza uvunaji haramu na uvunaji holela
- Kutoa elimu ya mazingira kwa vijana
- Kutoa elimu ya uhifadhi kwa vijana
- Kuanzisha mipango ya usimamizi shirikishi wa misitu

Kipindi cha 4: Haki za Jamii katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM)

MALENGO	Kufikia mwisho wa kipindi washiriki wataweza: Kujua haki zao katika usimamizi shirikishi wa misitu.
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Chati pindu • Kalamu kubwa • Gundi • Kitini: Haki za jamii katika USM (uk wa 5 katika Mwongozo wa ushirikishwaji wa jamii katika kuhifadhi misitu, Idara ya Misitu na Nyuki)
MUDA	Dakika 45
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi apitie njia za kupunguza matishio ya misitu kama yalivyoanishwa katika kipindi kilichopita na kulinganisha na washiriki wanachojua kuhusu haki zao juu ya rasilimali za misitu. 2. Mkufunzi atumie chati pindu zilizoandaliwa kufafanua haki za jamii juu ya rasilimali za misitu kulingana na mwongozo wa usimamizi wa misitu ya jamii ulioandaliwa na Idara ya Misitu na Nyuki. 3. Mkufunzi awambie washiriki kutoa maoni yao kuhusu haki za jamii katika USM. 4. Mkufunzi aandike maoni ya washiriki kwenye chati pindu akifafanua kila moja inapobidi. 5. Mkufunzi agawe vitini na kufafanua maneno muhimu yaliyojitokeza katika kitini. 6. Mkufunzi ahitimishe kwa kusisitiza kuwa jamii inayo haki ya kushiriki katika kusimamia rasilimali za misitu kwa faida yao lakini kwamba ili waweze kufanya hivyo, wanapaswa kusajili msitu wao na kupata idhini kutoka kwa serikali. Katika kipindi kinachofuata tutajadiliana zaidi kuhusu namna ya kufanikisha USM .
MAONI	<ul style="list-style-type: none"> • Mkufunzi anapaswa kuwa wazi na kuwakumbusha kuwa haki ni tofauti na majukumu. • Haki kimsingi ni 'yale wanayoweza kufanya na wasiyoweza kufanya kuhusiana na rasilimali za msitu'. • Majukumu ni 'mambo yale wanayopaswa kuyafanya'. • Maudhui ya kipindi hiki ni kufafanua haki zao. Katika kipindi cha 6 kuhusu hatua za uanzishaji wa USM, washiriki wataangalia zaidi kwa undani majukumu ya jamii katika USM.

Haki

Haki ni mambo ambayo unaweza kuchukua au kutoa. Kuna aina mbili za haki: haki za kimila na haki za kikatiba.

- **Haki za kimila**

Hizi ni haki ambazo zinaweza kuhamishika kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine m.f kupata maeneo ambayo yana muhimu wa kutambikia/kuabudia. Haki za kimila zinatofautiana kutoka eneo moja hadi lingine kutegemea na desturi za eneo husika.

- **Haki za kisheria au za kikatiba**

Hizi ni haki zinazotambulika kisheria, m.f haki ya kuishi, haki ya kupata elimu, na haki ya kulindwa. Kuhusiana na Usimamizi wa misitu ya jamii, Sheria za Ardhi ya Vijiji (1999), Sheria ya Serikali za Mitaa (1982), Sheria ya Misitu (2002), na Kanuni za Misitu (2004), zinatoa misingi ya sheria kwa wanakijiji kumiliki na kusimamia rasilimali za misitu zilizoko kwenye ardhi ya kijiji katika njia ambazo ni endelevu na zinazoleta faida.

Haki nyingine ni pamoja na:

1. Kukusanya madhuhuri kutoka mazao ya misitu. Hii inamaanisha kimsingi kuwa vijiji havina haja ya kufuata kiwango cha serikali za kukusanya mapato kutokana na mauzo ya mbao lakini wanaweza kuuza mazao hayo kwa bei wanayopendekeza na kukubaliana wao. (Sheria ya Misitu: Sehemu ya 78(3)).
2. Wanakijiji wanaweza kuunda na kutekeleza sheria ndogo za kulinda msitu wao
3. Wanakijiji wanaweza kutoza faini na kuzibakiza katika ofisi ya kijiji.
4. Wanakijiji wanaweza kuvuna mazao ya misitu kwa matumizi yao wenyewe (ili mradi yanaendana na mipango ya usimamizi wa msitu).
5. Wanakijiji wanaweza kuuza mazao ya misitu kwa watu wa nje wanaopendekezwa na wao wenyewe na kubakiza asilimia 100 ya mapato yote kijijini, hata hivyo hii haimaanishi kwamba kodi nyingine kama forodha na ongezeko la kodi zinapaswa kukwepwa.
6. Wanakijiji wanaweza kukamata mazao ya misitu na vifaa vilivyotumika katika uvunaji haramu katika ardhi ya kijiji chao; kuuza na kubakiza mapato yote.

Kipindi cha 5: Kanuni Muhimu za Kufanikisha USM

MALENGO	<p>Kufikia mwisho wa kipindi washiriki wataweza</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuelewa kanuni za msingi za usimamizi shirikishi wa misitu: • Kuwa na uwezo wa kuchambua hali halisi katika kijiji chao ili kuweza kuainisha kanuni ambazo hazijashughulikiwa • Kuweza kuainisha njia za kuweza kuwa na kanuni hizo katika kijiji chao.
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Chati pindu • Kalamu kubwa • Gundi • Kadi • Vijikaratasi vyenye nambari (1,2,3) • Kitini: Kanuni za Usimamizi Shirikishi wa Misitu.
MUDA	Saa 1 na dakika 30
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi aeleze madhumuni ya kipindi. 2. Mkufunzi awaeleze washiriki kuwa makundi matatu yataundwa kwa kila mshiriki kuokota kijikaratasi chenye nambari 1, 2 au 3 kilicho andaliwa. Nambari kwenye karatasi itaonyesha kundi lake. 3. Mkufunzi aorodheshe kanuni za usimamizi shirikishi wa misitu kwenye chati pindu. Mkufunzi atoe ufafanuzi na mifano kwa kila kanuni ya USM. Mkufunzi awambie washiriki kutoa mifano kwa kila kanuni kama njia ya kuongeza welewa wa kanuni hizi. 4. Mkufunzi atoe maelezo yenye ufafanuzi kwa kifupi kuhusu maana ya kanuni'. 5. Mkufunzi aviambie vikundi kuchagua kanuni 3 kutoka kwenye orodha ambazo zinakosekana katika kijiji chao na kupendekeza njia za kuweka kanuni hizo katika kijiji chao. Vikundi viandike kanuni hizo kwenye chati pindu. 6. Baada ya dakika 20, mkufunzi akaribishe mtu mmoja ajitolee kutoka kwenye kila kikundi kuwasilisha matokeo ya kikundi kwa kutumia chati pindu. 7. Mkufunzi aandike mambo muhimu kwenye chati pindu na kutoa muhtasari wake. 8. Mkufunzi aruhusu maswali kama yapo kutoka kwa washiriki kwa ufafanuzi zaidi. Mkufunzi ahitimishe kipindi kwa kutoa muhtasari wa kanuni za USM. Asisitize kuwa ni muhimu wote kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kuwa kanuni hizi zipo na zinafanyiwa kazi.
MAONI	<ul style="list-style-type: none"> • Wakati wa majadiliano, mkufunzi atembelee kila kikundi kusaidia majadiliano pale inapobidi. • Kanuni mara nyingi zinaweza kumaanisha tabia au mambo au hata vipengele maalum. • Washiriki wanaweza kuchagua kanuni zinazofanana. Baadaye mkufunzi anaweza kuandaa mawazo kutoka kwenye vikundi vingine.

Kanuni za msingi za kufanikisha USM

Ili Usimamizi shirikishi wa misitu kuwepo kuna kanuni za msingi ambazo zinapaswa kuwepo na zinahitaji kuheshimiwa. Kanuni hizi ni muhimu sana kama USM utakuwa endelevu na kuleta manufaa ya kweli kwa jamii. Kanuni hizi za msingi za USM zinajumuisha:

i) Upatikanaji wa Rasilimali

Kuanzisha USM kunahitaji rasilimali. Rasilimali hizi ni pamoja na; ardhi, misitu, rasilimali watu, na rasilimali fedha. Rasilimali fedha zinahitajika kuanzisha na kutekeleza USM kama vile kuandaa ramani, kufanya tathmini ya rasilimali, kujenga uwezo kuwezesha mikutano na kuhamasisha pamoja na kuongeza welewa.

ii) Uwepo wa sheria na sera thabiti

USM unalindwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998), Sheria ya Misitu (2002), Kanuni za Misitu za mwaka (2004), Sheria ya Ardhi ya mwaka (1999) na Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka (1982). Sera hizi, sheria na kanuni zinatoa mwongozo wa kisheria kwa vijiji kumiliki na kusimamia rasilimali za misitu kwenye ardhi za vijiji.

iii) Uwazi wa haki na miliki ya ardhi

Sheria ya Ardhi ya vijiji ya mwaka (1999) na Sheria ya Ardhi ya mwaka (1999) zinatoa mwongozo wa kisheria kwa vijiji kumiliki ardhi. Kuna aina tatu za ardhi nchini Tanzania. 70% ya ardhi ya Tanzania iko kwenye ardhi ya vijiji; 28 % ni ardhi iliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na Hifadhi za Wanyamapori, hifadhi nyingine, hifadhi za misitu; na 2% zinatambulika kama ardhi ya wazi ambayo iko mara nyingi kwenye maeneo ya Manispaa au maeneo ambayo yanamilikiwa na watu binafsi. Ardhi ya vijiji inaweza kutafsiriwa kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo yametengwa kuwa ardhi ya kijiji chini ya Sheria ya Miliki ya Ardhi (Matamko ya vijiji) ya mwaka 1965; au eneo ambalo limekubalika na Halmashauri za vijiji na Halmashauri za vijiji jirani; au eneo linaloelezewa kama ardhi ya kijiji kwenye cheti cha kijiji. Kwa kuwa vijiji vingi havina vyeti vya ardhi ya kijiji, ardhi hii bado ni ardhi ya kijiji kisheria. Kwa maana hiyo, vijiji vinaweza kuendelea kuanzisha Hifadhi za misitu ya vijiji hata kama kijiji hakina mpango wa matumizi bora ya kijiji au cheti cha kijiji.

iv) Utawala bora ulio thabiti

Utawala bora ulio thabiti unahitajika ili kuhakikisha USM upo. Utawala bora una maana ya uwajibikaji, uwazi, ushirikishwaji, uwakilishi, mawasiliano thabiti na demokrasia ya kuchagua viongozi.

v) Ushirikishwaji thabiti

Wanajamii wanapaswa kuhusishwa katika mchakato wa USM kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ushirikishwaji thabiti unaweza:

- Kuhamasisha umiliki
- Kuhakikisha uwazi
- Kupunguza migogoro
- Kujenga uwezo wa jamii
- Kuhakikisha uendelevu

vi) Kujenga uwezo wa Jamii

Kujenga uwezo wa jamii kunahitajika sana ili kuongeza welewa, kujiamini, na mbinu mbalimbali kwa jamii. Hii inaweza kufanikishwa kupitia mafunzo na kuhakikisha kwamba kamati za maliasili za vijiji, vikundi vya watumiaji na serikali za vijiji wanaweza kutumia ujuzi na mbinu wanazozipata kupitia mafunzo.

vii) Kutimiza mahitaji ya jamii

Usimamizi Shirikishi wa Misitu unahitaji kuendelezwa kwa namna ambayo inatambua haki na mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii hususan wanawake. Kwa mfano ni muhimu kuainisha makundi yote yanayotegemea misitu na kuyahusisha katika mchakato wa mipango. Ni muhimu hasa kuhakikisha kuwa wanawake na kaya masikini zinashiriki kuunda, kutekeleza na kufuatilia masuala ya usimamizi shirikishi wa misitu. Kila jitihada inapaswa kufanyika ili kuhakikisha kwamba mahitaji ya msingi kwa kaya masikini kwa mfano kuni bidhaa ndogo ndogo kutoka msituni, na malisho yanapatikana kutokana na mchakato wa mipango.

Haki za Jamii Katika Usimamizi wa Misitu (USM)



Kanuni nyingine za msingi za USM

- ✓ Utashi wa kisiasa
- ✓ Kutathmini na kusimamia kwenda na mabadiliko
- ✓ Kusimamia migogoro
- ✓ Uthabiti wa mgawanyo wa gharama na mapato

Kipindi cha 6: Hatua za Kuanzisha Usimamizi Shirikishi wa Misitu

MALENGO	<p>Kufikia mwisho wa kipindi washiriki wataweza</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kuelezea mpangilio ya mchakato wa USM; 2. Kutambua majukumu ya jamii katika kila hatua.
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Chati pindu • Kalamu kubwa • Gundi • Kadi: seti 3 za hatua za uanzishwaji wa USM kila hatua kwenye kadi moja. • Kitini: Mchakato wa uanzishwaji wa USM.
MUDA	Saa 1 na dakika 15
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi ahusishe kilichofundishwa kwenye kipindi cha 2: kuhusu 'mahusiano kati ta misitu na watu'; na kipindi cha 3 kuhusu 'majukumu ya jamii katika usimamizi endelevu wa misitu'. 2. Mkufunzi atoe utangulizi wa kipindi kwa kuelezea malengo ya kipindi. 3. Mkufunzi akaribishe washiriki kuwa kwenye vikundi vidogo vitatu na kwenye kila kikundi kutaka kila mshiriki kuhesabu nambari 1, 2 au 3. Nambari ambayo kila mmoja anahesabu inakuwa kundi lake. 4. Mkufunzi agawe seti moja ya hatua za kuanzisha USM kwa kila kundi bila maelezo na kila kundi liweke hatua hizo kwa mlolongo sahihi. 5. Mkufunzi aruhusu kila kundi kwa dakika 10 kuzipanga kadi hizo. 6. Kila kikundi kinapaswa kukubaliana juu ya mpangilio sahihi nakuwa na sababu ya mpangilio huo. 7. Baada ya dakika 10 mkufunzi awambie kila kikundi kuwasilisha mpangilio wao na sababu za msingi za mpangilio huo katika majadiliano. Makundi mengine yaulize maswali na ufafanuzi kama haja ipo. 8. Baada ya kila kundi kuwasilisha matokeo yao, mkufunzi aanzishe mjadala kulingana na maswali yafuatayo: <ol style="list-style-type: none"> a) Hatua ipi tunapaswa kuanza nayo? Kwa nini? b) Hatua ipi itapaswa kufuata? Kwa nini? c) Tunaweza kuona mpangilio ulio sahihi? d) Tunaweza kukubaliana juu ya hatua? e) Kuna mtu anaweza kuelezea mchakato mzima ulivyo? Mkufunzi anahitaji kutumia maswali yanayofanana ili kuwaongoza washiriki kupitia hatua za USM kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo wa Idara ya Misitu na Nyuki. 9. Mkufunzi apitie kwa ufupi kilichokubalika na kuruhusu washiriki kubadilishana ujuzi kuhusu ushiriki wao katika kila hatua. Majibu yaandikwe kwenye chati pindu. 10. Mkufunzi agawe kitini na kueleza kwa kifupi na kuruhusu maswali pale inapobidi. 11. Mkufunzi atoe muhtasari wa kipindi kwa kupitia hatua za USM na ushiriki wa jamii katika kila hatua.
MAONI	Baada ya kipindi, mkufunzi abandike hatua zote na kuonyesha ushiriki wa jamii katika kila hatua kwenye chati pindu. Chati pindu hizo zibandikwe kwenye chumba cha mafunzo kwa muda wote uliobaki wa mafunzo.

Hatua ya kwanza: Kuanza

Hii inafanyika katika ngazi ya Wilaya, kwa kuchagua vijiji. Inajumuisha kuwaeleza wataalamu wa wilaya kuhusu dhana na masuala ya USM; na kuunda timu ya wataalamu wa wilaya ikiwa ni pamoja na wataalamu wenye ujuzi mbalimbali unaohitajika katika uendelezaji wa USM. Katika ngazi ya kijiji, timu ya wilaya inakutana na Halmashauri ya kijiji na serikali ya kijiji ili kuwezesha uundaji wa kamati ya maliasili ya kijiji.

Majukumu ya jamii

1. Viongozi wa kijiji wanashiriki katika mikutano ya utangulizi wa USM wakiwa na maafisa kutoka wilayani.
2. Wanakijiji wote wanapaswa kuhudhuria na kushiriki katika mikutano ya hadhara ili kuelewa mchakato wa uanzishaji wa USM.
3. Wanakijiji wanachagua wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji.

Hatua ya Kwanza ya Uanzishaji Usimamisi Shirikishi wa Misitu (USM)



Hatua ya pili: Tathmini na Mipango ya usimamizi

Hapa ndipo wataalamu kutoka wilayani pamoja na wajumbe wa kamati ya maliasili wanaainisha na kuweka kumbukumbu za mipaka ya ardhi ya kijiji pamoja na mipaka ya misitu ya kijiji. Rasilimali za msitu zinapimwa au 'kutathminiwa'. Kutegemeana na matokeo ya tathmini iliyofanyika, mipango ya usimamizi inaundwa ikiwa pamoja na sheria ndogo za kijiji.

Hatua ya Pili ya Uanzishaji Usimamisi Shirikishi wa Misitu (USM)



Majukumu ya jamii

1. Kuainisha na kukubaliana kuhusu mipaka ya ardhi ya kijiji na mipaka ya hifadhi ya msitu wa kijiji uliopendekezwa.
2. Kamati ya maliasili inafanya Tathmini shirikishi ya rasilimali za misitu kwenye hifadhi ya msitu uliopendekezwa.


3. Kamati ya maliasili inaunda rasimu ya mpango wa usimamizi wa msitu na rasimu ya sheria ndogo.

Hatua ya tatu: *Kuhalalisha na kurasimisha USM*

Kamati ya maliasili ya kijiji inawasilisha rasimu ya mpango wa usimamizi wa msitu na rasimu ya sheria ndogo kwa Halmashauri ya kijiji na Serikali ya kijiji kwa ajili ya kupitishwa. Hizi zinawasilishwa kwa Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya kupitiwa na kupitishwa. Baada ya kufanya hivyo, kijiji kinaweza kuanza na hatua ya nne na kuanza kutekeleza mpango wao wa usimamizi wa msitu.

Majukumu ya jamii

- a) Wanakijiji wanashiriki katika mkutano mkuu wa kijiji kupitisha rasimu za mpango za usimamizi wa msitu na rasimu ya sheria ndogo.
- b) Kuwasilisha rasimu ya mpango wa usimamizi wa msitu na rasimu ya sheria ndogo kwa Halmashauri ya wilaya.



Hatua ya nne: *Kutekeleza mipango na sheria ndogo za USM*

Hapa ndipo jamii inaweka mifumo inayohitajika kusimamia misitu; kuteua na kutoa mafunzo kwa timu ya doria, kuanza kukusanya kumbukumbu na kuhakikisha kuwa sheria zinajulikana kwa wote, zinatekelezwa na kusimamiwa. Wilaya sasa inachukua jukumu la kufuatilia na kusaidia inapobidi na kadiri inavyoombwa na jamii.

Majukumu ya jamii

1. Kamati ya maliasili ya kijiji inahamasisha jamii ndani ya kijiji kuhusu utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa misitu wa kijiji na sheria ndogo.
2. Anza kulinda msitu
3. Anza uwekaji wa kumbukumbu muhimu na ufuatiliaji.
4. Simamia uvamizi wa misitu
5. Anza na shughuli za haraka za urudishaji wa msitu
6. Kusimamia hifadhi ya msitu wa kijiji unaoangukia katika vijiji zaidi ya kimoja.



Hatua ya Tano: Kupitia mpango wa usimamizi wa msitu, sheria ndogo na kutangaza hifadhi ya msitu wa kijiji kisheria

Baada ya miaka mitatu ya utekelezaji, jamii inapaswa kupitia upya mipango yao ya usimamizi wa msitu kulingana na maendeleo ya utekelezaji kwa wakati huo. Katika hatua hii, kijiji kinaweza kuanza kuomba rasmi Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Nyuki kutangaza msitu wao kuwa Hifadhi ya Msitu wa Kijiji katika gazeti za serikali. Hii ni hatua ambayo si ya lazima.

Majukumu ya Jamii

1. Kupitia mipango ya usimamizi wa misitu na sheria ndogo na kuainisha maeneo kwenye mpango au sheria ndogo ambayo yanahitaji marekebisho.
2. Kurekebisha mpango na sheria ndogo.
3. Kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho kwa Halmashauri ya wilaya.

Hatua ya sita: Kupanua shughuli kwenye maeneo mapya

Kijiji kinaweza kuamua kupanua shughuli za Usimamizi wa Misitu ya Jamii katika maeneo mengine kijijini. Upanuzi utaleta faida kwenye uboreshaji wa usimamizi wa misitu kwa maeneo makubwa zaidi.


Majukumu ya jamii

1. Kuelimisha kizazi kichanga na jamii zingine za jirani dhana za kuhusu USM kulingana na uzoefu wa jamii husika katika utekelezaji wa USM.
2. Fuatilia hatua ya 2, 3, 4 na 5 ili kupanua eneo la msitu chini ya usimamizi wa misitu ya jamii.

Hatua ya tano ya Uanzishaji Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM)



Hatua ya Sita ya Uanzishaji Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM)



Kipindi cha 7: Utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Mimitu

MALENGO	<p>Kufikia mwisho wa kipindi washiriki wataweza :</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuchambua faida na changamoto za utekelezaji wa USM. • Kuorodhesha wanachoweza kufanya ili kukabiliana na changamoto za USM.
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Kalamu kubwa • Chati pindu • Gundi • Kitini: Visa Mkasa vya USM 3
MUDA	Saa 1 na dakika 30
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Kwa muhtasari pitia walichojifunza kutoka vipindi vilivyopita kuhusu USM na hatua za uanzishaji wa USM. 2. Mkufunzi atoe utangulizi na madhumuni ya kipindi na kutoa maelezo juu ya USM katika Tanzania. Chukua maswali kwa ajili ya ufafanuzi. 3. Mkufunzi ataje kuwa USM una faida na changamoto zake. Kuwe na majadiliano kiasi kuhusu faida na changamoto za USM kwa ujumla. Faida zitakuwa ndiyo manufaa yanayopatikana kutoka msituni wakati changamoto zinaweza kuwa uwezo wa kijiji. 4. Mkufunzi aeleze kuwa tutaangalia visa mkasa kutoka maeneo mbalimbali ili kuainisha faida na changamoto za USM. Mkufunzi awagawe washiriki katika makundi matatu kwa kuhesabu namba 1, 2 hadi 3 na kuwapa kila kundi chati pindu. 5. Mkufunzi atoe maelezo mafupi kwa kila kisa mkasa (kama vile eneo la kijiografia kwa ujumla, USM ulipoanza n.k) lakini bila kwenda kwa undani zaidi. 6. Mkufunzi agawe kitini cha kisa mkasa kimoja kwa kila kundi (kisa mkasa namba 1 kwa kundi la kwanza, namba 2 kwa kundi la pili, na namba 3 kwa kundi la tatu) na waambie kuchambua faida na changamoto katika kila mfano wa USM. 7. Baada ya dakika 15, mkufunzi agawe mifano yote ya visa mkasa kwa washiriki wote na kuwambia mtu ajitolee kutoka kila kundi kuwasilisha matokeo yao. Fafanua na andika mambo muhimu yanayotajwa na wawasilishaji kwenye chati pindu ili kila mtu ayaone. 8. Pitia mambo muhimu moja baada ya moja kwa pamoja na washiriki na wahusishe uzoefu wao katika utekelezaji wa USM. 9. Katika majadiliano, mkufunzi awaambie washiriki watoe mawazo yao namna ya kukabiliana na changamoto hizo zilizoainishwa. Orodhesha maoni kwenye chati pindu na toa muhtasari wake. 10. Mkufunzi ahitamishe kipindi kwa kusisitiza kwamba ni muhimu kufanya kazi kwa pamoja ili kufanikisha faida za USM wakati huo huo kupunguza hasara zake.
MAONI	<ul style="list-style-type: none"> • Kama baadhi ya washiriki hawawezi kusoma na kuandika, mkufunzi anaweza kuwasilisha kisa mkasa kwa njia ya hadithi au kwa kumwambia mtu ajitolee kusoma kwa ajili ya watu wasioweza kusoma na kuandika. • Kama washiriki hawana uzoefu wowote na USM, wanaweza kufikiria kuhusu changamoto yoyote iliyopo au inayoweza kujitokeza katika siku za usoni. • Mkufunzi atoe ufafanuzi kwa kazi ya vikundi na kufuatilia maendeleo yake kwa karibu.

Hali ya sasa ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) katika Tanzania

- USM ni njia endelevu ya kusimamia misitu ambayo inakasimu majukumu ya usimamizi kwa watu binafsi, vikundi au jamii.
- Kuna aina mbili za USM nchini Tanzania: Usimamizi wa misitu ya jamii na Usimamizi wa Pamoja.
- USM umeenea kwa kasi sana na hadi sasa ni kama asilimia 10 ya eneo la misitu yote Tanzania.
- USM unatekelezwa katika wilaya 60.
- Utafiti unaonyesha kuwa misitu iliyoko chini ya USM inasimamiwa vizuri na jamii.
- Baadhi ya vijiji vinavyotekeleza USM vimeandaa mipango ya uvunaji endelevu na wameshaanza kupata kipato kutokana na kuuza mazao ya misitu.

- **Usimamizi wa Pamoja** ni njia ya ushirikiano katika usimamizi wa misitu ambapo jamii zilizoko kandokando mwa misitu wanafanya makubaliano ya usimamizi na mmiliki wa msitu (serikali au mtu binafsi) kuhusu usimamizi wa msitu.
- Umiliki wa msitu unabakia kuwa wa serikali au mtu binafsi, lakini manufaa/faida kama vile mbao, kuni na malisho yanaweza kuhamishwa kwa wanajamii husika kulingana na hali ya hifadhi (wa kuhifadhi au wa kuzalisha).
- Takribani hekta milioni 1.6 za misitu ziko kwenye mfumo wa usimamizi wa Pamoja katika vijiji 530.

- **Usimamizi wa Misitu ya Jamii** ni aina ya usimamizi wa jamii ambapo jamii ina majukumu yote ya kusimamia hifadhi ya misitu iliyoko kwenye ardhi ya kijiji. Kijiji kinafanya doria, kinatoza faini kwa uvunaji holela, kinachukua jukumu lote la utoaji wa leseni kwa ajili ya mazao ya misitu, kinabaki na mapato ya mazao ya misitu, kinatengeneza sheria ndogo na kanuni nyingine kuhusiana na usimamizi wa misitu pamoja na matumizi yake. Mapato ya misitu yanakusanywa na kamati ya maliasili ya kijiji na yanapangwa kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa misitu na maendeleo ya kijiji.
- Takribani hekta milioni 1.9 za misitu ziko chini ya Usimamizi wa Jamii katika vijiji 1500.
- Usimamizi wa Misitu ya Jamii unaahidi manufaa zaidi kwa jamii na maisha yao lakini katika hali nyingi faida hizi hazijaweza kuonekana.

Faida na Changamoto katika Utekelezaji wa USM:

- Pamoja na kwamba USM una faida nyingi kwa jamii, una changamoto nyingi sana ambazo zinazuia utekelezaji mzuri wa USM.
- Ili kuweza kuchambua na kuelewa changamoto za USM, ni muhimu kupitia baadhi ya mifano au kisa mkasa cha USM unavyotekelezwa.

Hekta 3000 za msitu wa Hifadhi wa kijiki cha Kikole uko chini ya Usimamizi wa Jamii.

- USM katika kijiki cha Kikole ulianzishwa mwaka 2002 chini ya ufadhili wa Idara ya Misitu na Nyuki kwenye programu ya USM.
- Kijiki cha Kikole kilijiunga na Programu ya USM baada ya kuambiwa juu ya faida zake na wataalam wa Wilaya.
- Serikali ya Kijiki (Mkutano mkuu) ulichagua kamati ya maliasili ya kijiki na kuanzisha sheria ndogo na mpango wa usimamizi wa msitu.
- Kupitia kamati ya maliasili ya kijiki, kijiki kinasimamia msitu kulingana na mpango wa usimamizi wa kijiki na sheria ndogo.
- Msitu unasimamiwa vizuri. Sheria ndogo zinatekelezwa kufuatana na doria zinazofanyika ndani ya msitu na wanakijiki.
- Kijiki kinavuna 'mpingo' na aina nyingine za miti kwa kufuata mpango wa uvunaji. Mapato kutokana na mauzo ya mbao yanasaidia kwenye maendeleo ya kijiki na usimamizi wa misitu.
- Mazao mengine ya msitu ukiacha magogo yanatumiwa na jamii kufuatana na mpango wa uvunaji ambao unazingatia uvunaji na matumizi endelevu ya msitu.
- Msitu umethibitishwa kimataifa. Sasa kijiki kinaruhusiwa kuuza mazao ya msitu. Pamoja na kwamba wanakijiki wanaweza kupata bei nzuri ya mazao ya msitu kutokana na kuuza bidhaa ambazo zimethibitishwa kimataifa, kuna wanunuzi wachache ambao wanaweza kumudu bei hiyo kwa sasa.
- Uboreshaji wa hali ya msitu pia unavutia makazi ya wanyama ambao pia wanavamia na kuharibu mazao ya kilimo kwenye mashamba ya wananchi.
- Kutokana na tofauti iliyopo ya masuala ya kijamii na kiuchumi kwa wanakijiki, sio kila mwanakijiki ameshiriki kufanya maamuzi kuhusiana na shughuli za USM.
- Maamuzi mengi ya usimamizi wa misitu yamefanyika na kundi la watu wachache hivyo hakuna michango kutoka kwa watu wengi.
- Kutokana na upungufu wa fedha na vipaumbele vya wilaya, inakuwa vigumu sana kupata usaidizi kutoka kwa wataalam wa wilaya.
- USM katika kijiki cha Kikole ulipata ufadhili kutoka kwa shirika la DANIDA, kwa kusaidiwa fedha za uwekezaji wa kuanzisha mchakato.
- Baadhi ya wanakijiki bado wanatumia moto kuandaa mashamba yao. Moto wakati mwingine unasambaa na kusababisha uharibifu wa mali za watu na hadi rasilimali za misitu.
- Baadhi ya watu bado wanaendelea kufyeka misitu kwa ajili ya kilimo cha kuhamahama pamoja na kuwepo kwa sheria ndogo

Faida na Changamoto katika Utekelezaji wa USM:

- Pamoja na kwamba USM una faida nyingi kwa jamii, una changamoto nyingi sana ambazo zinazuia utekelezaji mzuri wa USM.
- Ili kuweza kuchambua na kuelewa changamoto za USM, ni muhimu kupitia baadhi ya mifano au kisa mkasa cha USM unavyotekelezwa.

. Hekta 642 za msitu wa Kijiki cha Nndawa uko chini ya usimamizi wa jamii.

- USM katika kijiki hiki ulianzishwa mwaka 2002 chini ya Programu ya USM ya Idara ya Misitu na Nyuki.
- Kijiki cha Nndawa kilijunga na programu ya USM baada ya kupewa taarifa kuhusu faida zake na wataalam wa misitu wa wilaya
- Serikali ya kijiki ilichagua kamati ya maliasili ya kijiki na kutengeneza sheria ndogo za kijiki na mpango wa usimamizi wa msitu.
- Kupitia kamati ya maliasili ya kijiki, kijiki kinasimamia msitu kwa kufuata mpango wa usimamizi wa msitu pamoja na sheria ndogo.
- Msitu unasimamiwa vizuri, Sheria ndogo zinatekelezwa kupitia doria zilizopangwa kwenye mpango wa usimamizi wa msitu unaofanywa na wanakijiki.
- Wanakijiki wanavuna baadhi ya mazao ya mbao na yasiyo timbao kufuatana na mpango endelevu wa uvunaji.
- Misitu iliyoboreshwa inavutia wanyama ambao pia wanavamia mashamba ya wakulima.
- Jamii haina welewa kuhusu taratibu za uvunaji hakuna kipato kinachozalishwa na uvunaji wa mbao.
- Kutokana na tofauti iliyopo katika masuala ya kijamii miongoni mwanakijiki, ni vigumu kumhusisha kila mtu kwenye shughuli za USM
- Mara nyingi maamuzi kuhusu usimamizi wa misitu yanafanywa na watu wachache hivyo mawazo yanatoka kwa watu wachache.
- Kutokana na ukosefu wa fedha na vipaumbele vya wilaya, ni vigumu kupata usaidizi wa kutosha kutoka wilayani.
- USM katika Nndawa ulipata ufadhili kutoka wafadhili wa DANIDA ambao walitoa fedha kidogo kwa ajili ya kuanzisha mchakato.
- Baadhi ya vijiki vinatumia moto kuandaa mashamba yao. Moto wakati mwingine unasambaa na kuharibu mali ya watu na misitu pia.
- Baadhi ya watu wanaendelea kufyeka misitu kwa ajili ya kilimo cha kuhamahama

Faida na Changamoto katika Utekelezaji wa USM:

- Pamoja na kwamba USM una faida nyingi kwa jamii, una changamoto nyingi sana ambazo zinazuia utekelezaji mzuri wa USM.
- Ili kuweza kuchambua na kuelewa changamoto za USM, ni muhimu kupitia baadhi ya mifano au kisa mkasa cha USM unavyotekelezwa.

Hekta 3000 za msitu wa Kijiji cha Ihombwe uko chini ya usimamizi wa jamii.

- USM katika kijiji hiki ulianzishwa mwaka 2004 chini ya Programu ya USM ya Idara ya Misitu na Nyuki.
- Kijiji cha Ihombwe kilijiunga na programu ya USM baada ya kupewa taarifa kuhusu faida zake na wataalam wa misitu wa wilaya
- Serikali ya kijiji ilichagua kamati ya maliasili ya kijiji na kutengeneza sheria ndogo za kijiji na mpango wa usimamizi wa msitu.
- Kupitia kamati ya maliasili ya kijiji, kijiji kinasimamia msitu kwa kufuata mpango wa usimamizi wa msitu pamoja na sheria ndogo.
- Msitu unasimamiwa vizuri, Sheria ndogo zinatekelezwa kupitia doria zilizopangwa kwenye mpango wa usimamizi wa msitu unaofanyika na wanakijiji.
- Wanakijiji wanavuna baadhi ya mazao ya mbao na yasiyo timbao kufuatana na mpango endelevu wa uvunaji.
- Misitu iliyoboreshwa inavutia wanyama ambao pia wanavamia mashamba ya wakulima.
- Jamii haina welewa kuhusu taratibu za uvunaji hakuna kipato kinachozalishwa kutokana na uvunaji wa mbao.
- Kutokana na tofauti iliyopo katika masuala ya kijamii miongoni mwa wanakijiji, ni vigumu kumhusisha kila mtu kwenye shughuli za USM
- Mara nyingi maamuzi kuhusu usimamizi wa misitu yanafanywa na watu wachache hivyo mawazo yanatoka kwa watu wachache.
- Kutokana na ukosefu wa fedha na vipaumbele vya wilaya, ni vigumu kupata usaidizi wa kutosha kutoka wilayani.
- USM katika Ihombwe ulipata ufadhili kutoka wafadhili wa DANIDA ambao walitoa fedha kidogo kwa ajili ya kuanzisha mchakato.
- Baadhi ya watu wanaendelea kufyeka misitu kwa ajili ya kilimo cha kuhamahama

Hifadhi hii ya msitu iko mbali sana na makao makuu ya kijiji, hivyo shughuli nyingi za usimamizi wa msitu ni ngumu kutekeleza hasa za doria na ulinzi wa msitu kutokana na uchomaji wa mkaa na uvunaji wa mbao.

Moduli ya 2:

Mabadiliko ya Tabia nchi na Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa kutokana na ukataji wa miti na Uharibifu wa Mimitu (MKUHUMI).

Kipindi cha 8: Ushahidi na vyanzo vya Mabadiliko ya Tabia nchi	
MALENGO	Mwisho wa kipindi, washiriki watakuwa na uwezo wa: <ul style="list-style-type: none">• Kutumia njia za kawaida kuainisha ushahidi wa .• Kuainisha sababu za mabadiliko ya tabia kulingana na uzoefu wao.
VIFAA	<ul style="list-style-type: none">• Chati pindu• Kalamu kubwa• Gundi• Kadi• Kitini: ni nini? Ushadi wa mabadiliko ya tabia nchi ni nini?• Kitini: Sababu za mabadiliko ya tabianchi• Maana ya mabadiliko ya tabia nchi iliyoandaliwa kwenye chati pindu• Vijikaratasi vidogo ambavyo vimeandaliwa kwa kila washiriki kupata kimoja.
MUDA	Saa 1 na dakika 30
HATUA	<ol style="list-style-type: none">1. Mkufunzi aelezee kwa namna gani mabadiliko ya tabia nchi yameathiri maisha ya sasa hivi na mazingira kwa ujumla na kwamba hali ya hewa inabadilika na kuathiri kilamoja wetu na kusababisha matatizo kwa wanadamu. Mkufunzi aangalie kama kutoka kwa washiriki wana uwelewa wa kutosha kuhusu mabadiliko ya tabia nchi.2. Mkufunzi atumie chati pindu kuelezea nini mabadiliko ya tabia nchi na kuweka maana/tafsiri ya mabadiliko ya tabia nchi kwenye ukuta.3. Mkufunzi aelezee kwamba wakati wa kipindi hiki tutaangalia baadhi ya ushahidi wa mabadiliko ya tabia nchi. Mkufunzi awambie washiriki kufanya kazi kwenye vikundi 5 vilivyoainishwa na washiriki kwa kuhesabu 1 hadi 5 (waliohesabu 1 watenda kundi la 1 vivyo hivyo kwa wengine)4. Kilakundi kitumie dakika 15 kuorodhesha angalau ushahidi 3 wa mabadiliko ya tabia nchi kila ushahidi kwenye kadi moja.5. Mkufunzi amwambie mtu mmoja ajitolee kutoka kila kundi kuwasilisha ushahidi ulioainishwa na kikundi. Vikundi vinaambiwa kutorudia ushahidi uliyotajwa na vikundi vingine.6. Baada ya ya vikundi vyote kuwasilisha matokeo yao, mkufunzi atoe majumuisho ya namna mabadiliko ya tabia nchi yanavyo athairi maisha yetu. Mkufunzi aelezee kwamba ili kuepuka athari zaidi ya mabadiliko ya tabia nchi tunapaswa kupunguza visababishi vya mabadiliko ya tabia nchi.7. Mkufunzi awambie kila kundi kujadili kuhusu visababishi vya mabadiliko ya tabia nchi na kuandika kwenye kadi.8. Baada ya dakika 15, mkufunzi awambie kila kikundi kuweka kadi zao kwenye chati pindu bila kurudia. Uliza maswali kama inahitajika.

	<p>9. Mkufunzi aruhusu majadiliano kulingana na visababishi vya mabadiliko ya tabia nchi vilivyoorodheshwa kwenye kadi inapohitajika na kuongeza sababu zinazokosekana.</p> <p>10. Kutoka kwenye orodha ya sababu , mkufunzi ataje ukataji wa miti kama chanzo mojawapo cha mabadiliko ya tabia nchi. Mkufunzi aseme kwamba hatajifunza zaidi kuhusu kwa nini misitu yetu inatoweka na kwa namna gani upotevu wa misitu unachangia mabadiliko ya tabia nchi katika kipindi kijacho.</p> <p>11. Mkufunzi anahitimisha kipindi kwa kugawa vitini kwa washiriki na kuelezea mambo muhimu katika kitini.</p>
<p>MAONI</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kama washiriki hawawezi kuorodhesha angalau ushahidi wa aina 3 wa mabadiliko ya tabia nchi mkufunzi anaweza kuandaa picha/michoro inayoonyesha ushahidi huo wa mabadiliko ya tabia nchi na kuwauliza washiriki kama wanaitambua. • Kama baadhi ya yaliyo orodheshwa ni madhara na sio ushahidi wa mabadiliko ya tabia nchi m.f kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuenea kwa wadudu wa haribifu, mkufunzi anaweza kufafanua. • Madhara yanamaanisha matokeo yoyote ambayo yamesababishwa na mabadiliko ya tabia nchi kwa muda mrefu.

Maana ya Mabadiliko ya Tabia nchi

Mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya muda mrefu ya hali ya hewa yanayotokea katika sehemu maalumu, kanda au sayari. Mabadiliko haya yanapimwa kwa vithibitisho vinavyoendana na kiwango cha wastani wa hali ya hewa kama vile nyuzi joto, mwenendo wa upepo na mvua.

Ushahidi wa Mabadiliko ya Tabia nchi

Ushahidi wa mabadiliko ya tabia nchi umejadiliwa hapa chini:

Ongezeko la marudio ya matukio ya hali ya hewa
Ongezeko la marudio ya matukio ya hali ya hewa kama ukame na vimbunga vikali. Katika Tanzania, hali hii ya mabadiliko ya hali ya hewa yametokea katika baadhi ya maeneo kama Manyara.

- **Ukame.** Ukame mwingi na mkali zaidi umeonekana kwenye maeneo mengi tangu miaka ya 1970, hususan katika maeneo ya tropiki na nchi zilizo kusini mwa Sahara ya Afrika. Tanzania kama nchi nyingine zilizoko kusini mwa Sahara imeathirika na ukame katika baadhi ya maeneo.

Barafu za milimani na theruji zimepungua kwa wastani katika pande zote za dunia.


Vina vya bahari duniani vinaongezeka kwa kiwango cha takriban milimita 1.8 kwa mwaka.

Madhara ya Mabadiliko ya Tabianchi

Uzalishaji hafifu. Tathmini ya sasa ya madhara ya mabadiliko ya tabianchi inaonyesha kuwa baadhi ya mikoa inapata upungufu wa chakula kutokana na kupungua kwa uzalishaji hafifu katika kilimo kwa sababu za hali ya hewa isiyo tabirika, upungufu wa mvua na ongezeko la nyuzi joto.

Magonjwa yanayo ambukiza. Kwa sasa ugonjwa wa maleria umeongezeka katika maeneo kama Lushoto na Njombe, maeneo ambayo yalikuwa haya athiriki siku za nyuma kutokana na hali ya joto inayoruhusu mazingira ya mazali ya mbu.

Upotevu wa maisha na mali. Mafuriko, ukame na mvua ya vimbunga yote kwa pamoja yamesababisha kupotea kwa maisha na mali hususan miongoni mwa watu maskini zaidi.



Tabianchi inajumuisha mwenendo wa nyuzi joto, mvua, fukuto, upepo na majira; Mabadiliko ya tabianchi yanasababishwa na shughuliza binadamu ambazo zinatoa gesi joto katika anga. Shughuli hizi ni pamoja na:

Uchomaji wa mabaki ya kilimo

Moshi unaotokana na uchomaji wa mabaki ya kilimo au wakati wa matayarisho ya mashamba kwa ajili ya shughuli za kilimo ni moja ya vyanzo vya mabadiliko ya tabianchi.



Mbolea za kemikali

Katika mashamba yetu wakati mwingine tunatumia mbolea za kemikali kuboresha uzalishaji. Gesi joto zinaachiwa kwenda angani wakati wa utengenezaji wa mbolea hizi na kwa namna zinavyo changanyikana udongo.

Uzalishaji kutokana na viwanda na magari

Kuna viwanda vingi na magari duniani kote siku hizi. Moshi inayozalishwa na viwanda pamoja na magari inachangia sana mabadiliko ya tabianchi kwa kuachia gesi joto kama gesi ya ukaa



Uchomaji wa mkaa

Uchomaji wa miti kwa ajili ya utengenezaji wa mkaa unaachia gesi ya ukaa katika anga hivyo kuchangia katika mabadiliko ya tabianchi.

Ukataji wamiti kwa ajili ya mbao, uchimbaji wa madini na ufugaji

Ukataji wamiti kwa ajili ya mbao, mirunda, nguzo, maeneo ya malisho au uchimbaji wa madini unapunguza uwezo wa miti kunyonya gesi joto kama ya ukaa.

Moto

Matukio ya moto yanasababisha kuachia kwa gesi ukaa moja kwa moja kwenye anga.

Mifugo

Mifugo na wanyama wengine wanaachia gesi ya methane, moja ya aina ya gesi joto zenye hatari.



Kipindi cha 9: Vyanzo na njia za Kupunguza ukataji wa miti na uharibifu wa misitu

MALENGO	<p>Mwisho wa kipindi, washiriki wataweza kuwa na uwezo wa :</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kutofautisha kati ya ukataji wamiti hovyoy na uharibifu wa misitu. • Kutambua vyanzo vya ukataji wa miti na uharibifu wa misitu • Kuainisha njia za kupunguza ukataji wa miti na uharibifu wa misitu katika eneo lao. • Kuelezea njia nyingine za upunguzaji zinazoendelea katika maeneo mengine
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Chati pindu • Kalamu kubwa, • Gundi • Kitini: Vyanzo vya ukataji wa miti na uharibifu wa misitu • Kitini: Njia za kupunguza • Michoro au picha kwenye chati pindu zikionyesha tofauti kati ya ukataji wa miti na uharibifu wa misitu
MUDA	Saa 1 na dakika 30
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi awambie washiriki kukumbuka vyanzo vya mabadiliko ya tabianchi kutokana na vipindi vilivyopita na kusema kwamba katika kipindi hiki, tutaangalia zaidi kwenye vyanzo vya mabadiliko ya tabianchi vinavyohusiana na misitu. 2. Mkufunzi aeleze kwamba upotevu wa misitu unachangia uzalishaji wa gesi ya ukaa ambayo inasababisha mabadiliko ya tabianchi. 3. Mkufunzi awambie washiriki kwamba kuna aina mbili za upotevu wa misitu na kuwaonyesha washiriki michoro au picha za ukataji wa misitu na uharibifu wa misitu. 4. Mkufunzi aelezee maana ya Ukataji wa miti hovyoy na uharibifu wa misitu kwa kutumia picha/michoro. Elezea kuwa kila njia ya upotevu wa miti kwa kuikata inahitaji njia tofauti ya kuizuia. 5. Kama maswali yakijitokeza kutoka kwa washiriki, ndipo mkufunzi anaweza kutoa ufafanuzi/majibu 6. Waambie washiriki kuunda vikundi 3 vidogo kwa kuhesabu 1 hadi 3. Washiriki watakaohesabu nambari 1 wanaunda kundi la kwanza, hivyo makundi mengine. 7. Waambie washiriki kutoa majibu ya maswali, "kwa nini misitu yetu inatoweka au iko katika hali mbaya?", Je tutazuia je hali ya upotevu na uharibifu wa misitu siku za usoni?". Kwa kila chanzo cha ukataji wa miti au uharibifu wa misitu, vikundi vinapaswa angalau kutoa njia moja ya kupunguza hali hii. Ruhusu dakika 20 kwa ajili ya majadiliano na andika kwenye chati pindu. 8. Waambie washiriki kuandaa jedwali kama linavyoonekana hapa chini:




Vyanzo vya uharibifu wa misitu	Njia ya kupunguza hali hii	Vyanzo vya ukataji wa miti	Njia za kupunguza

9. Mkufunzi amwambie mtu moja ajitolee kutoka kila kundi kuwasilisha matokeo yao bila kurudia majibu yaliyokwisha tajwa
 10. Ruhusu majadiliano na ufafanuzi kulingana na mawasilisho.
 11. Mkufunzi atumie chati pindu kuelezea njia nyingine za kupunguza hali hii (muhtasari kutoka kwenye kitini) zinazotumika katika maeneo mengine kwa maelezo kidogo
 12. Mkufunzi agawe vitini kwa washiriki na kutoa ufafanuzi wa masuala muhimu katika kitini kwa kulinganisha yaliyomo kwenye kitini na matokeo ya majadiliano wakati wa kipindi.
 13. Mkufunzi ahitimishe kipindi kwa kuhamasisha washiriki kuhakikisha wanepuka vyanzo vya kataji wa miti hovyoyote na uharibifu wa misitu kwa kuwa zinachangia sana kwenye mabadiliko ya tabianchi.

MAONI	<ul style="list-style-type: none"> Mkufunzi anapaswa kuwa na uwelewa wakutosha juu ya njia mbalimbali za kupunguza hali ya uharibifu na ukataji wa miti na kuwa na uwezo wa kutoa mifano.
--------------	--

Ukataji misitu



maana ya ukataji misitu ni " uondoaji wa kudumu wa eneo la msitu na ubadilishwaji wa matumizi kutoka kwenye matumizi ya msitu, iwe kwa makusudi au kwa kudhamilia."



HAKUNA MITI

Uharibifu wa misitu

Uharibifu wa misitu unamaanisha mabadiliko ndani ya msitu ambayo huathiri vibaya muundo au kazi ya msitu, na hivyo kupunguza uwezo wa utoaji wa huduma na mazao za msitu.



BAADHI YA MITI HUBAKI


Tofauti kati ya Ukataji miti na uharibifu wa misitu ni kwamba ukataji miti husababisha aridhi kutumika kwa matumizi mengine kabisa, wakati uharibifu wa misitu, msitu utabaki kama msitu lakini wenye faida na ubora usioridhisha (mdogo sana).

Sababu ya ukataji miti na uharibifu wa misitu ni kama ifuatavyo.

Vyanzo vya uharibifu wa misitu *	Sababu za ukataji miti (misitu)
Uzalishaji wa mkaa	Ukaji misitu kwa ajili ya Kilimo cha biashara
Uvunaji mbao	Kwa shughuli nyingine za maendeleo kwa mfano; mabwawa, hoteli, migodi nk
Cutting poles and withies Kukata miti na fito	Settlement Makazi
Ufugaji wa kupita kiasi	Uendelezaji wa miundombinu
Uzalishaji wa mazao katika vivuli vya msitu mfano iliki.	Ukataji wa misitu kwa ajili ya kilimo kidogo cha kudumu
Kilimo cha kuhamahama	

* Baadhi ya shughuli zilizo orodheshwa kama sababu za uharibifu wa misitu pia husababisha ukataji miti (misitu) kama zitafanyika kwa kiwango kikubwa kwa mfano, katika suala la kilimo cha kuhamahama, kama muda wa vipindi vya kilimo hautoshelezi kuwezesha msitu kujitotesha tena, hii inakuwa ukataji msitu badala ya uharibifu wa misitu.

Sababu za uharibifu wa misitu



Uharibifu wa misitu na ukataji miti ni moja ya sababu za mabadiliko ya tabianchi. Ili kupunguza mabadiliko ya tabianchi tunahitaji kuzuia uzalishaji zaidi wa gesi joto. Njia moja ya kufanya hivyo ni kupunguza ukataji miti na uharibifu wa misitu.

Baadhi ya shughuli ambazo wanawake na wanaume wanaoishi vijijini Tanzania wanaweza kufanya ili kuzuia ukataji miti na uharibifu wa misitu na pia kuleta faida nyingine kwa jamii ni kama yafuatayo:

- **Kuandaa na kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji**

Kuwa na matumizi bora ya ardhi ya kijiji ni mpango muhimu kwa ajili ya haki ya kumiliki ardhi na kwa ajili ya matumizi endelevu ya maliasili. Kukiwa na mpango mzuri wa matumizi ya ardhi, jamii inaweza kutenga ardhi yao kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile kilimo, malisho, usimamizi wa misitu, maeneo ya makazi, huduma za jamii kama vile zahanati, shule na maeneo ya soko. Kutekeleza mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji kwa ufanisi kunahitaji ushirikishwaji na nia ya jamii na wadau wengine wenye maslahi ya ardhi hiyo. Kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi pia husaidia kijiji kupata cheti cha Ardhi ya Vijiji ambayo ni hatua muhimu kuelekea kupata haki ya kumiliki ardhi.

- **Kutumia njia bora za kilimo endelevu**

Ukataji wa misitu na uharibifu mwingi unaotokea katika ardhi za vijiji Tanzania kwa sababu ya kilimo. Kwa kutumia mbinu bora za kilimo, wakulima wanaweza kuongeza uzalishaji kutoka mashamba yao wanayoyatumia na hivyo kuepuka haja ya kuhama na kuanzisha mashamba mengine. Mbinu bora za kilimo ni pamoja na hatua za kuhifadhi ardhi, kilimo mseto, umwagiliaji na matumizi ya mbegu bora. Haya hutegemea mahali na aina ya mazao yatayolimwa.



Kilimo mseto



Kufunika ardhi moja kwa moja

- **Usimamizi Shirikishi wa Misitu**

Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM) ni neno la jumla kuelezea ushiriki wa jamii katika usimamizi wa misitu. Utunzaji wa misitu ya jamii ni aina moja ya mbinu USM inayofanyika katika ardhi ya kijiji, katika misitu ambayo inamilikiwa au kusimamiwa na Halmashauri ya Kijiji kwa niaba ya serikali ya Kijiji na inapelekea kuwa na Hifadhi ya Misitu wa Kijiji, Hifadhi ya Misitu ya Kijiji au Hifadhi ya Misitu binafsi.


- **Kupanda miti na kutumia majiko banifu**

Kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kuni kwenye misitu ya asili kwa kupanda miti kama chanzo endelevu cha kuni na kwa kutumia majiko banifu.

- **Utoaji elimu**

Elimu ya mazingira ni muhimu katika kujenga uwezo wa jamii juu ya usimamizi endelevu wa misitu. Kuwa na elimu ya mazingira, watu watakuwa na uwezo wa kusimamia rasilimali za asili hizo ambazo maisha yao hutegemea sana.

- **Kuanzishwa kwa shughuli nyingine za uzalishaji mali**



Kupunguza msukumo mkubwa kwenye misitu, jamii inapaswa kutafuta mafunzo ya shughuli mbadala za mapato. Wanakijiji wanahaja ya kujua na kuelewa rasilimali zilizopo katika maeneo yao ambayo zinaweza kuwasaidia kuzalisha vipato mbadala. Shughuli hizi zinaweza kuwa ni pamoja na utalii, kilimo cha uyoga na miradi ya ufugaji nyuki.

- **Utekelezaji wa sheria**

Halmashauri ya kijiji na wanakijiji wote lazima wafuate sera, sheria na sheria ndogondogo zinazohusiana na misitu ili rasilimali za misitu zitumike vizuri.

- **Utaratibu wa MKUHUMI**

MKUHUMI ni motisha ya kifedha uliopendekezwa katika Mkutano wa Mataifa 2005 kwenye mkutano wa kimataifa wa Mwongozo wa Umoja wa Mataifa wa Mkataba wa Mabadiliko ya tabianchi uliofanyika mjini Montreal. MKUHUMI unalenga kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa na gesi joto nyingine zinazotokana na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu kwa kutoa motisha ya kifedha kwa nchi zinazoendelea kuhifadhi misitu yao.

Kipindi cha 10: MKUHUMI na Hifadhi za Kaboni

MALENGO	<p>Mwisho wa Kipindi, washiriki wataweza:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kueleza maana ya MKUHUMI na MKUHUMI +. • Kutaja hifadhi 6 za kaboni • Tofautisha ipi ni kaboni na ipi si kaboni • Orodhesha na kueleza vipengele muhimu ya MKUHUMI
VIFAA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Chati pindu 2. Kalamu Kubwa 3. Kitini: Hifadhi za kaboni 4. Kitini: Vipengele vya MKUHUMI 5. Kitini: Uhusiano kati ya MKUHUMI, USM na Mabadiliko ya tabianchi 6. Kadi
MUDA	Saa 1 na dakika 30
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi atoe utangulizi na madhumuni ya kipindi na arejee njia mbalimbali za kukabiliana na ukataji miti na uharibifu wa misitu Mkufunzi atumie chati pindu 2. Mkufunzi atumie chati pindu kuelezea kwa kifupi kuhusu MKUHUMI na MKUHUMI + (kwa muhtasari / kwa maana zaidi rejea Kitini) na kuruhusu maswali kwa ufafanuzi zaidi 3. Mkufunzi arejee maana ya MKUHUMI na MKUHUMI+ kama motisha ya kifedha kwa ajili ya kupunguza uzalishaji wa gesi ukaa kutokana na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu. 4. Mkufunzi aelezee kuwa upotevu wa misitu ni chanzo kikubwa cha uzalishaji wa hewa ukaa. Hivyo katika kipindi hiki tutajifunza mahali ambapo kaboni ina hifadhiwa ndani ya misitu. Eneo hili hujulikana kama hifadhi ya kaboni (carbon pools). 5. Kwa msaada wa mchoro wa mti, Mkufunzi anaelezea maeneo mbalimbali ambapo kaboni huifadhiwa. 6. Mkufunzi anaruhusu majadiliano na maswali kuhusu (carbon pools) hifadhi za kaboni. 7. Mkufunzi anafanya zoezi kuangalia uelewa wa washiriki na kusambaza kadi zilizoandikwa vitu mbalimbali kama iliyotolewa katika Kitini mfano, jiwe, mwamba, mkaa, karatasi, kuni, majani, shina la mti, majani, kioo, bati, plastiki, mzoga nk . mshiriki mmoja mmoja aambiwe kuweka kadi katika safu sahihi ama ni kaboni au sio kaboni 8. Baada ya kumaliza zoezi hilo, mkufunzi alianzisha majadala kuhusiana na matokeo na kufanya marekebisho inapobidi. 9. Mkufunzi ataje kwamba ili kuuza kaboni kutoka katika misitu yetu, tunahitaji kujua/ kufahamu vipengele vitatu ya msingi ya MKUHUMI

	<ol style="list-style-type: none"> 10. Mkufunzi anatoa vipengele vitatu ya msingi (ongezeko, uvujaji, na hali ya ukudumu) mmoja baada ya nyingine na mkufunzi ataangalia ni kwa kiasi gani washiriki wameelewa maana ya kila kipengele kwa kuuliza maswali. 11. Mkufunzi anatumia chati pindu kueleze maana ya vipengele vitatu vya MKUHUMI, kimoja baada ya kingine (rejea Kitini). 12. Mkufunzi anasaidia washiriki kuonesha uhusiano wa vipengele vitatu vya MKUHUMI kwa kila mmoja kwa kuwauliza maswali 13. Mkufunzi anahitimisha kwa kuwaambia kwa nini vipengele hivyo vitatu ni muhimu katika mradi wa MKUHUMI. 14. Mkufunzi inasambaza Kitini na anaelezea mambo muhimu katika Kitini. 15. Mkufunzi anapitia upya maana ya MKUHUMI, na MKUHUMI +, umuhimu wa hifadhi ya kaboni na vipengele muhimu ya MKUHUMI kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi (rejea Kitini). Mkufunzi anawakumbusha washiriki upotevu wa msitu ni chanzo kikubwa cha ongezeko la hewa ukaa na utachangia katika mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri maisha yetu. Ilikupunguza mabadiliko ya tabia nchi, tunapaswa kutunza kaboni kwa kuhifadhi misitu vizuri. Wafahamisha washiriki kwamba MKUHUMI bado upo katika hatua za majadiliao katika ngazi za kitaofa na kimataifa. Taratibu na miuundo bado ina andaliwa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. Sote tunahitaji kujiandaa ili MKUHUMI kuwa tayari kutekelezwa katika eneo letu 16. Mkufunzi anatumia mchoro kuonesha uhusiano kati ya MKUHUMI, USM na mabadiliko ya tabianchi na kuhitimisha kipindi
<p>MAONI</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Mkufunzi anatakiwa kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu MKUHUMI katika ngazi ya kitaifa na ngazi nyingine. • Kwa taharifa zaidi kuhusu MKUHUMI katika Tanzania, tafadhali tembelea tovuti hii www.reddtz.org au www.tnrf.org / REDD

MKUHUMI(REDD) ni nini?

MKUHUMI(Mpango wa kuzupunguza gesi ukaa inayotokana na ukataji wa miti na Uharibifu wa Misitu)

MKUHUMI ni mfumo wa kifedha uliopendekezwa katika Mkutano wa 2005 wa Vyama (COP 11) Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mkataba wa Mabadiliko ya tabianchi katika Montreal. MKUHUMI una lengo la kupunguza uzalishaji wa gesi joto zinazotokana na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu kwa kutoa motisha ya kifedha kwa mataifa yenye misitu kutunza au kusimamia misitu yao vizuri. MKUHUMI unatoa nafasi ya kutumia fedha kutoka nchi zilizoendelea kupunguza ukataji miti (misitu) katika nchi zinazoendelea. MKUHUMI unaweka thamani katika misitu kwa ajili ya huduma zitolewazo na misitu hiyo kwa kuweza kunyonya hewa chafu kutoka angani.

MKUHUMI +

MKUHUMI + unasimama kwa ajili ya kupunguza uzalishaji hewa ukaa kutokana na ukataji wa misitu na uharibifu wa misitu na kuendeleza/kuimarisha hifadhi na kiwango cha kaboni. Alama ya '+' katika MKUHUMI + inapanua wigo wa utaratibu na kujumuisha **uhifadhi na kuimarisha uhifadhi wa kaboni kwenye misitu ikiwa pamoja na usimamizi endelevu** wa misitu. Hii inamaanisha kwamba shughuli kama vile usimamizi mzuri wa maeneo ya hifadhi, mashamba ya miti, uboreshaji, na kupunguza madhara ya magogo bado hayajawa vipengele vya mikakati ya MKUHUMI +. Maana ya usimamizi endelevu wa misitu hauko wazi vizuri. Hata hivyo, maana hii inaweza kuelezea zaidi shughuli nyingi za usimamizi wa misitu ya kijamii zinazofanyika na jamii za vijijini.

Kupanua wigo wa MKUHUMI kuwa MKUHUMI + kwa ujumla huonekana kama hatua chanya kwa nchi zinazoendelea. Hata hivyo, kuna baadhi ya hoja kwamba MKUHUMI+ itafungua mlango kwa ajili ya maslahi ya viwanda kudai kiasi cha kaboni kilichopungua wakati wakiendelea kutumia misitu kwa njia isiyo endelevu (RECOFTC, 2010).

Faida za MKUHUMI kwa jamii zinazotegemea misitu ni pamoja na malipo ya moja kwa moja kutokana na utunzaji wa misitu, ajira, mafunzo ya usimamizi wa maliasili, na kuendelea kwa matumizi ya misitu kwa ajili ya kuboresha hali ya maisha na matumizi ya kitamaduni. Shughuli za MKUHUMI zinafanyika kwa muda na faida zitaendelea kwa miongo kadhaa.

Vipengele vya MKUHUMI

MKUHUMI unahitaji watekelezaji kuonyesha kuwa ukataji miti na uharibifu wa misitu umepungua kabisa. Kufanikisha hili kunahitaji taarifa za kina kuhusu eneo la aina mbalimbali za msitu na ujazo wa kaboni kwa misitu hiyo pamoja na hatari ya kuwa msitu ungeweza kukatwa

Tafiti zilizofanyika hapa nchini na kwingineko zimeweza kuweka thamani kwenye kiwango cha kaboni kilichopo mfano. Hifadhi za misitu. Hata hivyo, labda kama kuna tishio kwa msitu husika kwamba msitu nzima ungeweza kufyekwa huo msitu huwezi kufaulu kwa uzima wake kwa malipo ya MKUHUMI. Kuna vipengele vitatu muhimu ambayo vinahitaji kuangaliwa wakati wa kupanga kwa ajili ya MKUHUMI. Navyo ni: -

Ongezeko: Changamoto za msingi katika muundo wa MKUHUMI ni kuonyesha ongezeko "additionality". Ongezeko kwa urahisi katika MKUHUMI huelezwa kama ni punguzo hewa ya ukaa ambalo lisingetokea bila kuwepo kwa muundo wa MKUHUMI. Ili kupunguza

mabadiliko ya tabianchi, ni lazima kuwe na nyongeza inayotokana na kupunguzwa kwa hewa ukaa itakayo uzwa katika soko la kaboni.

Uvujaji unamaanisha kutegemea kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi joto kusikotarajiwa nje ya mipaka ya mradi kutokana na shughuli za mradi (IPCC, 2008). Hii inaweza kujitokeza endapo upunguzaji wa ukataji wa miti katika eneo moja unahamisha shughuli za ukataji wa miti katika eneo lingine.

Kuna aina mbili za uvujaji katika shughuli za MKUHUMI ambazo ni: uvujaji wa shughuli na uvujaji wa soko

Uvujaji wa shughuli hutokea wakati shughuli ambayo ilisababisha ukataji miti katika eneo la mradi inapelekwa eneo ambalo ni nje ya mipaka ya eneo la mradi. Kwa mfano, wakulima ndani ya eneo la mradi wa uhifadhi wanaweza kuhamisha shughuli zao za kilimo nje ya eneo la mradi.

Uvujaji wa Soko hutokea wakati mradi au sera zinapo badilisha uwiano wa usambazaji na uhitaji, na kusababisha watendaji wa masoko kuhama. Kwa mfano, kama mradi utapunguza upatikanaji wa mbao, bei zitapanda, na zitasababisha upatikanaji wa mbao katika eneo lingine na ukataji wa miti katika eneo nje ya mradi zitaifikiwa kwa usambazaji kuongezeka (na kuongezeka kwa ukataji miti) kutoka nje ya eneo la mradi.

Kudumu unahusiana na muda wa matokeo chanya ya shughuli za kupunguza mabadiliko ya tabianchi. Udumu una maanisha kwamba haya matokeo yatadumu kwa muda usiojulikana.

Wakati tukizingatia kuwa kupunguza utoaji hewa ya ukaa ni wa kudumu, swali la msingi ni kwamba je kiwango cha hewa ukaa kinapungua katika anga baada ya kuwapo kwa hizi sera? Udumu hivyo unazingatia sana kiwango cha uzalishaji wa kiasi cha hewa ukaa katika anga.



Hatari katika udumu ni pamoja na:

- Hatari za *kiikolojia*: moto, majanga ya asili, ugonjwa;
- Hatari za *kiserikali*: mabadiliko katika serikali huweza kuleta mabadiliko katika vipaumbele vilivyo wekwa;
- Hatari katika mahitaji (*soko*): Kama thamani ya bidhaa shindani (kama vile mawese) ikiwa juu (ikiongezeka), hifadhi ya kaboni inaweza kuacha kuwa na faida. Kupunguza hatari hiyo na sababu zinazopelekea ukataji miti lazima zieleweke na kutafutiwa ufumbuzi katika sera ya taifa na mazungumzo ya kimataifa.

Masoko ya hiari na ya lazima: Katika kipindi cha kuandaa muongozo huu (2011), Masoko ya kaboni kutokana na MKUHUMI yanaweza kununuliwa na kuuzwa katika masoko ya hiari tu. Hii ina maana kwamba soko lipo kwa makampuni ambayo kama sehemu ya kuwajibika kijamii na kimazingira wangeweza kupunguza uzalishaji wao wa gesi ukaa. Hawawezi kutumika kuelezea/kuonyesha msimamo wa nchi chini ya Makubaliano ya Kyoto. Kwa mfano, kampuni inayozalisha umeme inaweza kununua kaboni ili kufidia uzalishaji wao wa gesi ukaa. Ili hewaukaa kuweza kuuzwa, ni lazima kuthibitishwa na mpango unaokubalika. Mpango unaotumika sana ni mpango wa hiari wa kaboni (VCS). Katika mazingira ya MKUHUMI, hii mara nyingi inaendana na Uthibitishaji wa miradi kupitia mpango wa Mabadiliko ya tabianchi, Jamii na bioanuwai ambayo inaonyesha kwamba kaboni inayouzwa imepatikana katika njia ambayo imezingatia masuala ya kijamii na kimazingira.

Maswali ya mara kwa mara kuhusu MKUHUMI?

Kwa nini ni MKUHUMI unafanyika katika nchi zinazoendelea na si katika nchi zilizoendelea?

Nchi zilizoendelea zinazalisha zaidi gesi chafu kuliko nchi zinazoendelea kwa sababu uchumi wao hutegemea zaidi shughuli za viwanda na magari. Nchi nyingi zilizoendelea zina misitu kidogo hivyo viwango vya ukataji miti ni vidogo sana. Badala yake, nchi zilizoendelea zinatafuta ufumbuzi na njia ya kupunguza uzalishaji gesi chafu kutoka katika sekta viwanda, magari, na uzalishaji wa umeme. Kuna njia nyingi za kupunguza uzalishaji wa gesi joto. MKUHUMI ni mfano mmoja tu ambao ni muhimu zaidi kwa jamii ya Tanzania. Kwa sababu nchi zilizoendelea zinatoa gesi joto zaidi kuliko nchi zinazoendelea, ni nchi zilizoendelea ambao zina fadhili MKUHUMI.

Tukiwa Kama wanakijiji (wanajamii) wa kawaida, ni jinsi gani tunaweza kuuza kaboni?

Utaratibu wa kupima kaboni iliyopo, kukadiria punguzo la gesi ukaa, na kuuza hewa ukaa iliyopatikana katika masoko ya kaboni ni mgumu. Jamii inahitaji msaada wa kiufundi kufanikisha hili. Pia haieleweki vizuri namna MKUHUMI utakavyoendeshwa katika siku zijazo na bei ambayo itakubalika kwa kaboni. Nchini Tanzania, MJUMITA, Mtandao wa jamii wa usimamizi wa misitu Tanzania umeanzisha mradi wa majaribio ya kusaidia jamii kuuza kaboni yao. Kwa habari zaidi kuhusu suala hili wasiliana na MJUMITA (www.mjumita.org).

- **Mwanakijiji binafsi anaweza je kuuza kaboni kwa njia ya MKUHUMI kama anamiliki msitu wake?**

Inawezekana kwa mwanakijiji binafsi kuuza kaboni katika soko la kaboni lakini ili kuwa na faida, ardhi ya misitu ambayo inamilikiwa na mtu binafsi lazima iwe kubwa sana ili gharama zilizotumika kufanya uhakiki na uthibitisho ziweze kurudishwa na mapato yatakayo tokana na mauzo ya kaboni. Ni bora zaidi kwa jamii ya kufanya kazi kwa pamoja ili waweze kuuza kaboni yao kwa pamoja na hivyo mapato hayo yanaweza kugawanywa katika jamii.

Hifadhi za Kaboni katika misitu


Ikiwa MKUHUMI ni mpango wa motisha ya kifedha ambayo ina lengo la kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa katika anga, tunahitaji kuelewa mahali ambapo kaboni inahifadhiwa katika misitu yetu.

Kaboni ni muundo wa kemikali. Ni ya nne kwa uwingi duniani (kwa tungamo). Kaboni hupatikana katika aina zote za viumbe hai, ikiwa ni pamoja na wanyama, binadamu miti na nyasi. Ni kemikali ya msingi wa uhai wa kila kiumbe.


Hifadhi ya kaboni katika misitu ni mahali katika msitu ambapo kaboni huifadhiwa. Maeneo matano ambapo kaboni inahifadhiwa na:

- i. Juu ya ardhi, hii ni pamoja na majani ya matawi, vigogo mti, vichaka, mimea, nyasi, vidandizi na wanyama wanaoishi juu ya ardhi.
- ii. Miti iliyokufa: hizi ni kuni zilizo oza, kuni zilizokufaa zinazopatikana juu ya ardhi kama vile matawi ya miti.
- iii. Majani yaliyoanguka hii inajumuisha kuanguka kwa majani ya miti, vichaka, na vidandizi, juu ya ardhi na kuunda safu kama blanketi juu ya sakafu ya msitu.
- iv. Chini ya Udongo, hii ni pamoja na aina zote za mizizi ya miti, mimea vidandizi, na mimea inayo patikana chini ya ardhi pamoja na wanyama wanaoishi katika udongo.
- v. Mboji ya Udongo: hii inajumuisha mboji iliyochanganywa kwenye udongo kama vile majani yaliyooza au mizoga ya wanyama ambayo ni sehemu ya udongo.

Misitu inachangia katika mabadiliko ya tabianchi kama haisimamiwi katika hali endelevu. Kwa mfano, wakati mti unavunwa unaacha kuhifadhi hewa ya ukaa (kaboni). Hii ina maana kuwa hakuna tena kunyonya hewa ya ukaa katika anga. Aidha, wakati msitu unaharibiwa kaboni iliyo hifadhiwa hutolewa kama hewa ukaa (CO₂).



Uhusiano kati ya usimamizi shirikishi wa misitu (USM), MKUHUMI na Mabadiliko ya tabianchi



Herufi hizo hapo juu zinawasilisha yafuatayo:

A : USM utajenga msingi kwa ajili ya utekelezaji wa MKUHUMI nchini Tanzania kwa ajili ya misitu ya jamii na misitu ya serikali inayo simamiwa kwa pamoja na jamii. Motisha inayo tokana na MKUHUMI baada ya kuuza kaboni itasaidia kuimarisha usimamizi shirikishi wa misitu USM.

B: MKUHUMI utapunguza uzalishaji wa hewa ukaa (CO_2) kwa njia ya kuzuia ukataji miti na uharibifu wa misitu na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Hii hasa itafanikiwa baada kukabiliana na vitu vinavyo sababisha kuwepo kwa ukataji miti na uharibifu wa misitu.

C: Mabadiliko ya tabianchi yanaweza kuleta athari katika misitu ya Tanzania. Baadhi ya mabadiliko ambayo yanaweza kutokea ni pamoja na mabadiliko katika aina ya muundo wa aina ya viumbe, kupungua kwa bioanuwai na mabadiliko katika mazingira msitu kutokana na moto na magonjwa. Mambo haya kwa upande mwingine yanaweza kuathiri bidhaa na huduma za misitu ambazo jamii hutegemea.

Kipindi 11: Hitimisho na Tathmini

MALENGO	<p>Mwisho wa Kipindi:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Wakufunzi kuelewa kiwango cha uelewa wa washiriki kuhusu yaliyokuwemo katika mafunzo <ul style="list-style-type: none"> • Washiriki wamependekeza njia za kuboresha mafunzo.
VIFAA	<ul style="list-style-type: none"> • Chati pindu • Maswali 4 yaliyotayarishwa kwenye chati pindu, kila swali moja kwa kila chati pindu. • Viti au nafasi.
MUDA	Saa 1
HATUA	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mkufunzi anaeleza madhumuni ya kipindi na maelezo ya jinsi njia ya mchezo wa 'bakuri la samaki' (fish bowl) unavyo fanya kazi.. 2. Mkufunzi anawakaribisha washiriki wasimame na wapange viti vyao katika duara mbili (mduara wa ndani na mzunguko wa nje). Idadi ya viti katika mzunguko wa ndani lazima iwe robo ya jumla ya washiriki na ziada moja. 3. Mkufunzi anawakaribisha robo ya washiriki wakae katika mduara wa ndani na anaeleza kuwa mkao huo ni sawa na ule wa samaki aliye kunjwa hivyo wao ni kama samaki. Kiti kimoja kitakuwa wazi. Robo tatu ya washiriki iliyobaki wanatakiwa kukaa katika mzunguko wa nje kama binadamu. 4. Mkufunzi anaeleza kuwa samaki wanaweza kuzungumza kwa sauti kubwa lakini binadamu hawaruhusiwi kuzungumza. Binadamu lazima wasikilize kwa makini. 5. Mkufunzi anauliza swali la kwanza na samaki kutakiwa kujibu. Mtu yeyote kutoka mduara wa nje anayetaka kuchangia lazima akae katika kiti kilichowazi. Baada ya kuchangia hutakiwa aondoke kwenye kiti na kurudi sehemu yake ya awali. 6. Mkufunzi anawapa dakika kumi kwa samaki kujibu swali. 7. Wakati samaki wanajadili, Mkufunzi anaandika mambo muhimu yanayo jadiliwa katika chati pindu ili kila mtu kila mtu aweze kuona. 8. Baada ya dakika 10, mkufunzi anakaribisha samaki wapya kukaa katika mzunguko wa ndani. Mchakato huu hurudiwa hadi maswali yote yatakapo isha. 9. Mkufunzi anafanya mapitio ya mambo muhimu yaliyojiri katika mjadala, na kufanya kufafanua haja inapobidi. 10. Mkufunzi anahitimisha na kuwashukuru washiriki wote kwa ushirikiano wao walio uonyesha.
MAONI	<p>Mkufunzi anaweza kunyambulisha maswali kama inafaa.</p> <p>Maswali manne ni:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kwa nini usimamizi wa misitu ya jamii ni muhimu kwa mwanakijiji wa kawaida? 2. Jinsi gani unaweza kushiriki katika usimamizi wa misitu ya jamii? 3. unaelewa nini kuhusu MKUHUMI 4. Tufanye nini ili kuboresha mafunzo haya katika siku za usoni?

Njia za kutengeneza vikundi

1. Kukutana na wageni

Bainisha ukubwa wa kundi, waombe watengeneze kundi lenye watu wasiofahamiana.

2. Makundi yenye mambo ya kufanana

Kundi hili hukaa pamoja na kundi la kawaida au kundi la watu wenye ufahamu; mfano wajumbe wa halmashauri kuu ya kijiji, wakulima au waganga wa jadi.

3. Viatu, kola, nk

Angalia uwezekano wa kutumia kitu chochote kilicho karibu kutengeneza makundi kama ya kuvaa:

- o Kahawia, nyeusi au vyenye rangi
- o Blauzi yenye mikono mirefu, blauzi yenye mikono mifupi na fulana
- o Miwani na bila miwani.

4. Mashua ina zama!

Kuwaelezea kuwa wao ni abiria katika mashua inayozama na hivyo wanatakiwa kutengeneza kundi kulijaza kwa idadi itakayokubalika.

Kuita: mashua inazama tengenezeni kundi la watu sita kujaza mashua isizame.

5. Mchezo wa mnyama

Mchezo huu husaidia kugawanya kundi kubwa katika vikundi vidogo vidogo. Wape kipande cha karatasi kila mtu katika kikundi. Andika jina la mnyama juu ya kila kipande cha karatasi, andika majina mengi ya wanyama mbalimbali kwa kadiri unavyohitaji vikundi vidogo vidogo vingi. Toa karatasi bila mpangilio na kuwambia watu kufanya kelele za wanyama wao ili kupata wanachama wengine wa kundi dogo.

Viburudisha/vichangamsha mwili

1. Linganisha kadi

Mwezeshaji anateua idadi ya misemo maalumu, na anaandika nusu ya maneno kwenye kipande cha karatasi au kadi. Kwa mfano, kuandika 'Happy' juu ya kipande cha karatasi na 'Birthday' juu ya karatasi nyingine. (Idadi ya vipande vya karatasi lazima ilingane na idadi ya washiriki katika kundi.) Weka vipande vya karatasi vilivyokunjwa kwenye kofia. Kila mshiriki anachukua kipande cha karatasi kutoka katika kofia na anajaribu kutafuta mjumbe mwenye maneno yanayolingana kiasi.

2. Kachumbari ya Matunda

Mwezeshaji anawagawa washiriki katika idadi sawa ya matunda matatu au manne, kama vile machungwa, ndizi na nazi. Washiriki kisha wanakaa kwenye viti katika mduara. Mtu mmoja lazima asimame katikati ya mzunguko wa viti. Mwezeshaji ana soma kwa sauti jina la moja ya matunda, kama vile 'machungwa, na wote wa

machungwa lazima wabadilishane maeneo na watu wengine. Mtu aliyesimama katikati anajaribu kuchukua sehemu ya kukaa wakati wengine wakiwa wanatembea, na kumuacha mtu mwingine katikati bila kiti. Mtu mpya katikati anasema kwa sauti tunda lingine na mchezo unaendelea. Wito wa 'kachumbari ya matunda' maana yake ni kwamba kila mtu anatakiwa kubadilisha viti.

1. Usijibu

Waambie washiriki wasimame katika duara. Mtu mmoja anatakiwa kwenda kwa mtu mwingine na kumuuliza swali kama vile, Je, tabia gani inayokuudhi sana? Hata hivyo, Hautakiwi kujibu swali mwenyewe – mtu ambaye yupo upande wa kushoto lazima ajibu. Watu wanaweza kufanya kujibu katika hali ya kufikiria wenyewe iwezekanavyo!

2. "Prrr" na "Pukutu"

Uliza kila mtu kufikiria ndege wawili. Mmoja anaitwa 'prrr' na mwingine anaitwa 'pukutu'. Kama wakiita 'prrr', washiriki wote watasimamia vidole vya miguu na kutakiwa kucheza mguu kwa upande wa pembeni, kama vile ndege anavyotanua mbawa zake. Kama wakiita 'pukutu', kila mtu anatakiwa kutulia na si kutanua miguu kama mbawa za ndege.

5. Nini kimebadilika?

Washiriki watengeneze jozi. Washiriki kuchunguzana na kujaribu kuutafakari mwonekano wa mwenzake. Kisha mmoja anarudi nyuma wakati mwingine anafanya mabadiliko matatu katika mwonekano wake, kwa mfano, kuweka saa zao mkono mwingine,, kuondoa miwani, na kuzungusha mikono yao. Mtu mwingine anajaribu kuangalia hayo mabadiliko matatu. Kisha wachezaji wanabadilishana majukumu.

SEHEMU YA 4 VIAMBATISHO

Kiambatisho cha 1. Maelezo

Ongezeko	Kiasi halisi kinachopimika kwa muda mrefu cha upungufu wa uzalishaji wa hewa ukaa ambacho kisingetokea bila kuwepo kwa mradi
Bioanuwai	Jumla ya aina mbalimbali ya wanyama, mimea na viumbe hai vidogo vidogo vinavyoishi duniani ikiwa ni pamoja na tofauti zao za kimaumbile.
Tungamo ya majani	Jumla ya tungamo la viumbe hai.
Kaboni	Ni aina ya kemikali ambayo ni msingi wa viumbe hai. Inapoachiwa katika anga inajiunda kuwa gesi ukaa, gesi ambayo inachangia mabadiliko ya tabianchi.
Gesi ukaa	Gesi inayoachiwa kutokana na kaboni na vimelea vyake katika anga ikiwa kama gesi ya kaboni
Usimamizi wa misitu ya Jamii	Mbinu ya usimamizi wa misitu ambayo hufanyika katika maeneo ya misitu katika ardhi ya kijiji. Inahusisha uanzishwaji wa misitu ya hifadhi ya kijiji(VLFR), misitu ya hifadhi ya jamii(CFR) au msitu wa hifadhi wa binafsi.
Mabadiliko ya tabianchi	Mabadiliko makubwa katika hali ya hewa hutokea kwa kipindi kirefu (kwa miongo) kutokana na tofauti ya asili au shughuli za binadamu.
Unyonyaji wa gesi ukaa	Ni uondolewaji wa gesi ukaa kwenye anga. Miti na mimea mingine inayonyona gesi ukaa kutoka angani kupitia mfumo wa usanidinuru
Hifadhi ya kaboni	Ni hifadhi ya gesi ukaa kama vile juu ya ardhi
Vipimo vya kaboni	Ni kipimo ambacho kinatumika kuuza gesi ukaa katika soko la kimataifa.
Soko la Kaboni	Ni soko lolote ambalo biashara ya kaboni inafanyika mara nyingi ni kwa njia ya vipimo vya kaboni
Ukataji wa miti	Ni badiliko la muda mrefu au la kudumu la ardhi yenye msitu kuwa ardhi isiyo na msitu
Uharibifu wa misitu	Mabadiliko ndani ya msitu ambayo huathiri vibaya muundo au kazi ya misitu na kupunguza kiasi cha kaboni inayohifadhiwa.
Uvamizi	Ukataji wa sehemu ya msitu kwa ajili ya kilimo au makazi.
Msitu	Eneo la mimea inayoongozwa na miti.
Hifadhi ya Msitu	Ni eneo la misitu ambalo limetengwa na linalindwa kisheria kwa ajili ya uzalishaji wa mbao na mazao mengine ya misitu au kwa ajili ya utunzaji wa bioanuwai na vyanzo vya maji.

Tangazo kwenye gazeti la serikali	Taarifa ya kisheria <i>katika ngazi ya taifa</i> kwenye Gazeti la Serikali kutangaza kwamba msitu unahifadhiwa kisheria.
Gesi Joto	Gesi ambazo zinasababisha mabadiliko ya tabianchi kwa kuhifadhi joto kutoka juani. Hewa ukaa ni mfano wa gesi joto.
Usimamizi wa misitu ya pamoja	Ni aina ya mfumo wa usimamizi wa misitu ambao unahusisha jamii katika usimamizi wa misitu wa pamoja na kati ya serikali kuu au serikali za mitaa.
Uvujaji	Ni ongezeko la uzalishaji wa gesi chafu katika eneo moja kama matokeo ya kukabiliana na hatua katika eneo lingine.
Kukabiliana	Shughuli ambazo zinalenga kupunguza uzalishaji wa gesi chafu katika anga.
Udumu	Muda na kutorudia kwa kupungua kwa uzalishaji wa gesi joto
Usimamizi Shirikishi wa Misitu:	Kusimamia rasilimali za misitu ambayo inasimika majukumu ya usimamizi kwa watu binafsi, kikundi au wanajamii.
MKUHUMI	Ni njia ambayo ilipendekezwa katika mkutano wa Mataifa (COP 11) wa mwaka 2005 kwenye mkutano wa Makubaliano ya umoja wa mataifa juu ya Mabadiliko ya tabianchi mjini Montreal, ambao ulilenga kupunguza uzalishaji wa gesi joto unaotokana na ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu kwa kuwapa motisha ya kifedha nchi zinazoendelea kuhifadhi au kusimamia kwa njia endelevu misitu yao.
MKUHUMI+	Alama ya '+' kwenye MKUHUMI+ inapanua wigo wa njia hii na kujumuisha uhifadhi na uendelezaji wa kiwango cha gesi ukaa katika msitu, pamoja na usimamizi endelevu wa misitu.
Msitu wa Hifadhi katika ardhi ya kijiji	Msitu ambayo iko ndani ya eneo la kijiji na inamilikiwa na jamii kwa ujumla na kutangazwa kama eneo la msitu wa hifadhi wa halmashauri ya kijiji na kuidhinishwa na mkutano wa Kijiji.
Kamati ya Maliasili ya Kijiji	Kamati ambayo ilichaguliwa na Mkutano wa Kijiji na kupitishwa na halmashauri la Kijiji kama msimamizi wa msitu wa hifadhi wa Kijiji.

Rejea

Angelsen, A (2008) Moving ahead with REDD: Issues, options and implications. CIFOR, Bogor, Indonesia, 156pp.

Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, 2009 Muongozo wa Taifa wa Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Gesi ukaa itokanayona na ukataji wa misitu na uharibifu wa misitu. (MKUHUMI), uk 38

Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, 2007, Muongozo wa Usimamizi wamisitu ya Jamii, uk 54

Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, 2007 Muongozo wa Usimamizi wa Misitu ya Pamoja, uk 57

Kiambatisho cha 3. Rasimu ya Ratiba

Mafunzo katika ngazi ya kijiji kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Misitu, Mabadiliko ya Tabianchi na Mpango wa Kupunguza uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na ukataji wamiti na uharibifu wa misitu”

MALENGO YA MAFUNZO

- Washiriki watakuwa wanaweza kuelezea dhana za Usimamizi Shirikishi wa Misitu na Mpango wa Kupunguza Ukataji wa miti ovyo na Uharibifu wa Misitu na mahusiano yaliyopo kati yao.
- Washiriki watakuwa wanaweza kuelezea hatua za kuanzisha Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM).

Siku ya 1

Muda	Mada	Malengo	Shughuli
03:00-03:30	Utangulizi wa mafunzo	Ifikapo mwisho wa kipindi hiki, washiriki wataweza: <ul style="list-style-type: none"> Kufahamiana Kufahamu malengo ya mafunzo Kukubaliana juu ya kanuni na taratibu za mafunzo.	Mawasilisho Kadi za manilia Majadiliano ya watu wote
03:30-04:15	Mahusiano kati ya watu na misitu	Ifikapo mwisho wa kipindi kila mshiriki ataweza kuorodhesha na kuelezea nini watu wanachopata kutoka kwenye msitu na nini msitu unachokipata kutoka kwa watu.	Kazi ya vikundi Mawasilisho
04:15-04:45	Mapumziko ya chai		
04:45-05:45	Majukumu ya jamii katika usimamizi endelevu wa misitu	Ifikapo mwisho wa kipindi hiki, washiriki wataweza: Kutambua nini wanakijiji wanaweza ili kuendeleza na kuongeza faida zitokanazo na msitu	Vikundi vidogo vya majadiliano
05:45-06:30	Haki za wanajamii katika USM	Ifikapo mwisho wa kipindi hiki, kila mshiriki ataweza kutambua haki zake katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu	Kuwasilisha majadiliano ya pamoja
06:30-07:30	Chakula cha mchana		
07:30-09:00	Kanuni za msingi za kufanikisha USM	Ifikapo mwisho wa kipindi washiriki wataweza kutambua kanuni za Usimamizi Shirikishi wa Misitu zinazokosekana katika maeneo yao na kuanisha fursa zilizopo na kuzitumia kuondoa pengo lililopo.	Kadi Vikundi vidogo vya Majadiliano Majadiliano ya pamoja
09:00-09:15	Mrejesho	Ifikapo mwisho wa kipindi hiki, muwezeshaji atakuwa ameelewa:- <ul style="list-style-type: none"> Hisia za washiriki kuhusiana na kipindi iliyofundishwa 	
09:15	Mwisho wa siku ya 1	Jinsi gani washiriki wamelewa kipindi ya siku hiyo	

Siku ya 2

MUDA	MADA	MALENGO	SHUGHULI/ZOEZI
03:00-03:15	Marudio ya masomo ya siku iliyopita	Ifikapo mwisho wa kipindi hiki: Washiriki watakuwa wamejadili na kujikumbusha masomo ya siku iliyopita	Margolish wheel
03:15-04:30	Hatua za USM	Ifikapo mwisho wa kipindi washiriki watakuwa na uwezo wa kuelezea hatua za Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa mpangilio ulio sahihi.	Kadi za manilia Kazi ya vikundi vidogo Majadiliano ya watu wote
04:30-05:00	Mapumziko ya chai		
05:00-06:30	USM katika utekelezaji	Ifikapo mwisho wa kipindi washiriki wataweza (i) kuchambua faida na changamoto katika utekelezeshaji wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu. (ii) kuorodhesha mambo wanayoweza kufanya ili kukabiliana na changamoto hizo.	Mifano ya USM Kazi ya vikundi vidogo Majadiliano ya watu wote
06:30-07:30	Chakula cha mchana		
07:30-09:00	Ushahidi wa mabadiliko ya Tabia nchi na mambo yanayosababisha mabadiliko hayo	Mwisho wa kipindi washiriki watakuwa na uwezo wa : Kutumia uwezo wao katika kutambua ushahidi wa mabadiliko ya tabia nchi. Kuainisha mambo yanayosababisha mabadiliko ya tabia nchi.	Kufikiria na kufanya kazi pamoja kwenye vikundi vidogo Majadiliano ya watu wote
09:00-09:15	Mrejesho nyuma	Ifikapo mwisho wa kipindi hiki, muwezesheji atakuwa ameelewa:- Hisia za washiriki kuhusiana na kipindi iliyofundishwa Jinsi gani washiriki wameelewa kipindi ya siku hiyo	mpira
09:15	Mwisho wa siku ya 2		

Day 3

MUDA	MADA	MALENGO	SHUGHULI/ZOEZI
03:00-03:15	Marudio ya masomo ya siku iliyopita	Ifikapo mwisho wa kipindi hiki: Washiriki watakuwa wamejadili na kujikumbusha masomo ya siku iliyopita	Mpira mwepesi (Beach ball)
03:15-04:45	Mambo yanayosababisha ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu na namna ya kuyapunguza	Ifikapo mwisho wa kipindi, washiriki wataweza: <ul style="list-style-type: none"> - Kutofautisha kati ya ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu - Kutambua visababishi vya ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu - kuainisha njia za kupunguza ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu kuelezea njia nyingine za kupunguza ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu zinazotumika maeneo mengine	Kazi ya vikundi vidogo Majadiliano ya watu wote
04:45-05:15	Mapumziko ya chai		
05:15-06:45	MKUHUMI na Hifadhi ya kaboni	Mwisho wa mada washiriki wa mafunzo waweze:- Kuelezea maana ya MKUHUMI <ul style="list-style-type: none"> ✓ Kutaja sehemu 6 ambazo kaboni huhifadhiwa ✓ Kutofautisha vitu ambavyo ni kaboni na visivyo kaboni ✓ Kuorodhesha na kuelezea masuala muhimu ya MKUHUMI msitu Kuorodhesha na kuelezea mambo muhimu ya MKUHUMI	Mawasilisho, Maswali na majibu, Zoezi
06:45-07:45	Chakula cha mchana		
07:45-08:45	Tathmini na hitimisho	Mwisho wa mafunzo mwezesheji atakuwa:- <ul style="list-style-type: none"> • ameelwa kama washiriki wameelewa mada zilizotolewa kwenye mafunzo. Ampata maoni ya washiriki yatokayowezesha uboreshaji wa mafunzo ya aina hii.	Fish bowl kujadili maswali manne(4)
08:45	Mwisho wa mafunzo		



Kuhusu Shirika La Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) ni Asasi isiyo ya kiserikali nchini Tanzania, iliyosajiliwa mwaka 1985, lina mwelekeo wa kuhifadhi na kurudishia misitu yenye wingi wa bioanuwai muhimu duniani na Tanzania kwa manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadaye. Hii itafanikishwa kupitia kujengea uwezo, uraghabishi, utafiti, maendeleo ya jamii na usimamizi wa maeneo yaliotengwa, katika njia ambazo ni endelevu na zinazozingatia ushirikishwaji, ushirikiano na ubia.

TFCG ina miaka 25 ya uzoefu katika utendaji wa masuala yanayohusiana na uhifadhi wa misitu Tanzania. Kupitia programu zake tano: uraghabishi, Usimamizi shirikishi wa misitu, elimu ya mazingira, maendeleo ya jamii na utafiti, TFCG imefanikiwa kuibua suluhu zenye ubunifu na zenye kuleta mafanikio kwa changamoto iliyopo katika misitu ya Tanzania na watu wanao itegemea. TFCG imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha uboreshaji wa usimamizi wa misitu na kupunguza ukataji wa miti hovyoka katika kipindi chote hiki. TFCG kwa sasa inafanya kazi kwa karibu na wilaya 14, vijiji 160 na karibu hekta 180,000 za misitu yenye wingi wa bioanuwai. Inasaidia katika nyanja za kujenga uwezo katika masuala ya usimamizi shirikishi wa misitu, kuboresha utawala katika ngazi za vijiji na kata, maendeleo ya jamii, uhamasishaji na kujenga welewa pamoja na elimu ya mazingira katika ngazi zote.

Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea www.tfcg.org

Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz



Kuhusu MJUMITA

Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) ni muungano wa vikundi vya kijamii vinavyoshiriki katika usimamizi shirikishi wa misitu Tanzania. Mtandao unatoa jukwaa kwa ajili ya kujengea uwezo, uraghabishi, mawasiliano na kutandaa kwa vikundi hivi. MJUMITA ilianzishwa na TFCG mwaka 2000 na imekuwa Asasi ya kujitegemea na kusajiliwa mwaka 2007. MJUMITA ilianzishwa kwa sababu kulikuwa na hitaji la kuwa na mahali jamii inapoweza kusemea na kubadilishana ujuzi na uzoefu kuhusiana na usimamizi shirikishi wa misitu na kuwa na majadiliano na Idara ya misitu na Nyuki ili kuweza kukabiliana na masuala muhimu ya kiseria, kisheria, na utekelezaji wa usimamizi shirikishi wa misitu. MJUMITA hadi sasa ina mitandao wanachama zaidi ya 80 ambayo inaundwa na wawakilishi wa kamati za maliasili za vijiji na vikundi vya mazingira. Mitandao ya ngazi ya chini inasajiliwa kisheria au iko mbioni kusajiliwa. Wanachama wa MJUMITA wanapatikana katika wilaya 23 na vijiji karibu 450.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea: www.mjumita.org

Barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org



Kuhusu RECOFTC

Welekeo wa RECOFTC ni kuona jamii wanasimamia misitu kwa uthabiti katika Ukanda wa Pasifiki wa Bara la Asia. Katika miongo miwili iliyopita RECOFTC imetoa mafunzo kwa zaidi ya watu 4,000 kutoka zaidi ya nchi 20 zinazosimamia misitu kwa njia shirikishi: kutoka watunga sera wa taifa, watafiti, na watekelezaji wa USM, na haki kupitia watumiaji wa misitu wa kawaida.

Huduma ya mafunzo na matukio ya kujifunza yanatokea kwenye miradi halisi inayotekelezwa, kuchambua masuala muhimu na mikakati ya mawasiliano.

Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea: www.recoftc.org

Barua pepe: info@recoftc.org